Jumatatu Mei 27, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • No. 0581689

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

**VIGOGO** serikalini washindwa kutaja vyanzo utajiri wao

UKURASA 3

**DK. BITEKO** atoa angalizo viongozi kutoheshimu mihimili iliyopo

UKURASA 2



**JELA** miaka 30 kuiba Tecno ya 660,000/-

UKURASA 7



**ENRIQUE: PSG ITASHINDA UEFA LICHA YA MBAPPÉ KUONDOKA**

UKURASA 22

UCHAGUZI UJAO

# Askofu Shoo aibuka na rushwa ya aibu

## Asema inapenyezwa hadi kanisani, Kinana aonya wapigakura kuchagua waliowatelekeza...

**MWANDISHI WETU,** MTWARA

"NDANI ya vyama vya siasa kuna migongano mikubwa kiasi kwamba wengi hawajui mwelekeo ni wapi, tatizo ni ubinafsi, kila mtu anaangalia mambo yake na si ustawi wa kundi, nchi na vizazi vyake.

Tuko pamoja kama kanisa ila kuna viongozi wameacha roho ya utumishi na kuangalia maslahi yao...'mungu pesa' ndiye amekuwa mungu wao badala ya kutumikia na kulisha kondoo wa Mungu na kusimama katika ukweli wa neno...

Endelea Uk. 2



Askofu Dk. Fredrick Shoo

## Msigwa, Sugu wachuana kwa hoja nzito uchaguzi CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

WAGOMBEA wa Uenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa na Joseph Mbilinyi 'Sugu' wameanza kuchuana kwa hoja nzito:

Sugu amedai amejitosa kwenye nafasi hiyo kutokana na msukumo wa wanachama ambao hawaridhishwi na uongozi wa sasa na hivyo kutaka mabadiliko.

Mch. Msigwa amesema hoja...

Endelea Uk. 3



Mbilinyi Msigwa

### YALIYOMO

UKURASA WA 5

**KUPAA DENI LA TAIFA**

**WATAKA WAZIRI WA FEDHA APUNGUZIWE MAMLAKA KUKOPA**

WADAU wa masuala ya madeni na maendeleo wameshauri serikali kushirikisha Bunge kabla ya kukopa ili kuondoa uwezekano wa mikopo kuishia...

**BAJETI YA ZIADA**

**Neema yawashukia wazabuni, watumishi Wizara ya Ardhi kulipwa madeni**

UKURASA 11-15

MICHEZO MABINGWA YANGA RAHA TU DAR UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

# Askofu Shoo aibuka na rushwa ya aibu

**Na Mwandishi Wetu,** MTWARA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Kikirsto Tanzania (CCT), Dk. Fredirick Shoo ameutaja ubinafsi ni sumu mbaya iliyofikisha baadhi ya watu kwenye hatua ya kutaka fedha chafu ili kupata madaraka na kujinufaisha kwa ustawi wao wenyewe badala ya maslahi ya taifa.

Amesema kwa kuendekeza ubinafsi taifa linafunga baraka zake zilizoahidiwa na Mungu, akitaka Watanzania kutumia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani kupata viongozi wanaojali maslahi ya wengi badala ya maslahi binafsi na familia yake.

Dk. Shoo ambaye Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini alitoa kauli hiyo jana wakati wa Ibada ya Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya CCT yaliyofanyika mkoani Mtwara.

Alisema ubinafsi umesambaratisha familia na kuleta madhara makubwa, ndani ya kanisa au usharika watu wanakusanyika lakini hakuna umoja ndani yao.

"Mafarakano ndani ya kanisa ni matokeo ya ubinafsi uliopitiliza na kutosimama na Mungu, unaharibu ustawi, mshikamano kwenye jamii ya watu kwa kuwa tunu ya Tanzania ni kutunza umoja. Inaamka roho ya kugawa watu kiukanda, ukabila ujue ibilisi ameingia na kupata nguvu.

"Ndani ya vyama vya siasa kuna migongano mikubwa kiasi kwamba wengi hawajui mwelekeo ni wapi, tatizo ni ubinafsi, kila mtu anaangalia mambo yake na si ustawi wa kundi, nchi na vizazi vyake. Tuko pamoja kama kanisa ila kuna viongozi wameacha roho ya utumishi na kuangalia maslahi yao...'mungu pesa' ndiye amekuwa mungu wao badala ya kutumikia na kulisha kondoo wa Mungu na kusimama katika ukweli wa neno.

"Hata kutumia njia za vitisho, udanganyifu ili kuwatisha watu watoe sadaka. Wanaojiita watumishi wa Mungu warudi katika wito wafanye kwa uaminifu. Si kujifanya mabwana au kutaka fedha ya aibu ili kupata madaraka fulani... tuwe na umoja, kusiwe na sauti mbili," alisema.

Alihimiza Watanzania kulipenda taifa na kuacha kujifikiria binafsi bali kuangalia ustawi wa nchi, kuona "tunataka Tanzania ya namna gani miaka 100 ijayo baada ya waliopo kuondoka?"

Askofu Dk. Shoo alieleza, "Viongozi wabinafsi tulionao ambao wanataka Tanzania iwe mali yao, chochote kinachopatikana ni kwa ajili yao na familia yao, 'kina hohehahe watajijua', ubinafsi ni sumu mbaya sana, tunaondoa baraka zilizoahidiwa kwa Tanzania."

Alisema mustakabali wa nchi unategemea umechagua kiongozi wa aina gani kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa, na ni wajibu wa kila Mtanzania kuangalia ni viongozi gani waadilifu na wacha Mungu na wenye kuipenda Tanzania na watoto wa Tanzania.

"Viongozi waadilifu, wacha Mungu hawa ndio tuwasukume, tuwachochee wagombee...ndivyo viongozi wazuri wanaofaa nchi wanavyopatikana. Usiangalie dini, madhehebu yao pale, kijijini unamfahamu, watu wema wanafahamika, hadi wilayani wanafahamika, watu hawa ndio tukawaweke na kuwapa madaraka ya kuongoza nchi.

"Tukalifanye kwa pamoja maana ni wajibu wetu, uamuzi mwingi unafanyika kwenye wilaya, halmashauri tukiwa na viongozi wabaya tunaishia kulalamika.

"Kwenye Uchaguzi Mkuu tunachagua wabunge ambao ndio wawakilishi wetu, unachagua mtu ambaye akishakanyaga lile jengo hajali alikotokea wala mahangaiko ya waliomchangua. Makosa ni ya nani? Ni wewe (mpigakura) uliyemchagua, tuchague ambaye atajali matakwa, maslahi ya anaowawakilisha bungeni. Maslahi ya taifa, tuache kukubali hongo," alisisitiza.



Askofu Shoo alisema kuna shida kubwa ya rushwa kwenye uchaguzi na kwamba ni mambo ambayo anatamani kusimama pamoja na watu wema bila kujadili dini, madhehebu kukataa rushwa katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

"Tukatae hata kama kuna mbunge amekuwakilisha sasa (miaka mitano) umeona ameweka maslahi ya waliomtuma (wananchi) mchague tena, lakini kama aliwasahau tangu 2020 anarudi mwaka huu na ujao akipita kwenye kila nyumba, mwambie 'sikujui kama ambavyo wewe hukunijua," alisema.

Askofu Shoo alisema wananchi walitoa maoni kuhusu Katiba Mpya, sheria za vyama vya siasa na zingine zinazohusu uchaguzi, lakini hajui ni kwa kiasi gani maoni yao, yakiwamo ya viongozi wa dini, yamezingatiwa.

"Ombi langu na wito wangu na sisi tunaopenda nchi yetu, kwa sauti ya pamoja tuseme viongozi madaraka na mamlaka, wabunge tuliowachagua mtuwakilishe, sikilizeni maoni yetu, heshimuni maoni yetu na myafanyie kazi. Kwa umoja tukipiga kelele kwa pamoja wataheshimu na kutekeleza," alisema na kuonya kuwa pasipo umoja hakuna amani, hakuna baraka kwa familia, kanisa na nchi.

**KINANA ALONGA**

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana naye ametaja sifa za kiongozi wanayemtaka ndani ya chama hicho kuwa ni anayekubalika kwa jamii, anayejituma, asiyetoa rushwa fedha na asiye na longolongo.

Aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, akisisitiza wabunge kuhakikisha wanaonekana majimboni. Wananchi wafunge milango kwa mbunge ambaye haonekani katika eneo lake la kazi. Ni kama ilivyo rai ya Askofu Dk. Shoo.

"Ukumbuke kwamba kabla ya kuja kuwa mheshimiwa kuna wengine walikuwa waheshimiwa, jambo lingine mbunge usiulizwe huyu tangu awe mbunge amefanya nini, kuwe na maendeleo yanayoonekana," alisema Kinana.

Alisema kuwa mambo yanayofanya CCM iendelee kudumu ni demokrasia ndani ya chama, akieleza kuwa siku wakivunja utaratibu huo ndani ya chama hali yao itakuwa mbaya.

"Wanachama wa CCM hakikisheni mnajua miradi yote ya maendeleo inayofanyika katika maeneo yenu ili ikifika wakati wa uchaguzi, msifanye kazi ya kukejeli na kutukana, hiyo si desturi ya chama chetu, kazi yetu ni kusimamia ilani ya CCM.

***Taarifa za ziada na Maulid Mmbaga**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE No. 11061 OF 2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**JULIUS GERVAS KAURA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**HAMIDA ISMAIL and ENES JULIUS KAURA**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of Probate Rules,Cap 352 R.E 2002)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above - named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of JUNE, 2024
Dated at Dodoma this 24 Day of May, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 10525/2024**
**In the matter of the Estate of the late**
**JACKSON LUHUSA MADULESI of Hombolo Makulu Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**MWIHUWILWA JACKSON MADULESI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of JUNE, 2024
Date at Dodoma this 06th Day of 4MAY, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## Biteko atoa angalizo viongozi kutoheshimu mihimili iliyopo

**Elizabeth John na Ibrahimu Joseph,** NJOMBE

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, amewataka viongozi kuheshimu utaratibu wa mihimili iliyowekwa kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi.

Dk. Biteko alielekeza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia katika Halmashauri ya Mji Njombe.

Alisema nchi inaongozwa na Katiba, muhimili mmoja hauruhisiwi kuingilia majukumu ya muhimili mwingine badala yake yote inafanya kazi kwa nia moja ya kuleta ustawi wa wananchi.

"Tuheshimu vyombo vyetu vya sheria, tufuate sheria kwenye maisha yetu. Nchi hii inaongozwa na Katiba na tumegawanya majukumu. Serikali ina majukumu yake, mahakama ina majukumu yake na Bunge lina majumuku yake, isitokee muhimili mmoja ukataka kuingilia majukumu ya muhimili mwingine," alionya.

Dk. Biteko alielekeza kuwa viongozi waliopo waheshimu utaratibu wa mihimili iliyopo na waache kuingilia vyombo vingine vya uamuzi kwa kutoa matamko kwa wananchi.

Pia alitaka wananchi kuacha misimamo iliyopitiliza wakati timu ya mawakili itakapokuwa inawasikiliza na badala yake wafuate ukweli.

"Maandiko yanasema ukijua kweli itakuweka huru, nawe utakuwa huru kwelikweli na mawakili simamieni ukweli mtapokuwa mnasikiliza watu hawa watakaokuja kwenu," alisema Dk. Biteko.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Haki Jinai ambayo lengo lake ni kuboresha mfumo wa upatikanaji haki kwa umma nchini.

"Tume ile ilikuja na mapendekezo, ilione mambo mengi ndani ya jamii ambayo migogoro mingi imo kwenye jamii, miongoni mwa migogoro hiyo ni ya ardhi, masuala ya mirathi na utawala bora, maana yake sisi viongozi tumekuwa sehemu ya migogoro hiyo," alisema Dk. Biteko.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema kuwa kupitia kampeni mbalimbali, jamii imeendelea kuelimika na kuhamasika.

Dk. Dorothy aliwataka wanaume kujitokeza kutoa kero zao ili kupata elimu itakayowasaidia kutotenda matukio ya kikatili.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, alisema tangu kuzinduliwa kwa kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia, mikoa saba imefikiwa. Hiyo ni Ruvuma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Manyara, Dodoma na sasa Mkoa wa Njombe.

Alisema katika mikoa sita, migogoro 516 imetatuliwa kati ya 4,942 na kufikia wananchi 4,15,000, akiwaomba wananchi wa Njombe kujitokeza kwa wingi ili kupata fursa ya msaada wa kisheri kupitia kampeni hiyo itakayofanyika kwa siku 10.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema mkoa huo umejiwekea utaratibu wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi na kampeni hiyo imekuja wakati mwafaka kwa kuwa itaongeza thamani kwa viongozi.

## HABARI KITAIFA

# Vigogo serikalini washindwa kutaja vyanzo utajiri wao

**Na Joseph Mwendapole**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imesema baadhi ya viongozi wamekwepa kutoa ufafanuzi wa vyanzo vya mapato waliyonayo na wameshindwa kutaja thamani ya mali walizonazo kwenye fomu ya tamko la mali.

Pia imesema baadhi ya viongozi wameshindwa kujaza taarifa za wenza wao hasa taarifa za fedha zilizoko benki na kukwepa kujaza vipengele muhimu, huku wengine wakipokea zawadi mbalimbali bila kuzitolea matamko.

Hayo yamo kwenye taarifa ya sekretarieti hiyo iliyowasilishwa mwishoni mwa wiki na Kamishna wa Sekretarieti hiyo, Sivangilwa Mwangesi, wakati akizungumza na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari juu ya mafanikio ya sekretarieti.

Alisema dosari hizo zinatoa taswira kwamba baadhi ya viongozi hawana uelewa wa kutosha kuhusu kujaza matamko ya mali na masuala yanayotakiwa kuainishwa.

Jaji Mwangesi alisema baadhi ya viongozi hutumia njia hiyo kuficha mali zilizopatikana kwa njia zisizo halali au kuwa na mali ambazo vyanzo vyake havina maelezo ya kutosha.

Alisema kutokana na dosari zilizojitokeza, sekretarieti ilichukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwataka viongozi kurekebisha matamko, kufanya uhakiki wa mali na madeni na kuendelea kutoa elimu kuhusu Sheria ya Maadili.

Jaji Mwangesi alisema hali ya urejeshaji matamko ya mali na madeni kwa viongozi inaridhisha. Kwa miaka mitano wastani wa urejeshaji umekuwa zaidi ya asilimia 96 kwa mwaka.

Alisema hali hiyo ni bora kulinganisha na asilimia 77 ya urejeshaji iliyokuwa katika kipindi cha miaka 10 iliyopita mwaka (2009 hadi 2020).

Alisema hali hiyo imesababishwa na juhudi za sekretarieti kutoa elimu juu ya Sheria ya Maadili na umuhimu wa kutoa tamko la rasilimali na madeni kwa makundi mbalimbali. Alisema hatua zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha viongozi wanafuata maadili nazo zimechangia kwa kiwango kikubwa kuwafanya viongozi kuwajibika kurejesha matamko kwa wakati.

Alisema hadi kufikia Juni mwaka 2023, jumla ya matamko 13,485 sawa na asilimia 87 ya matamko 15,556 yalipokewa na kufanyiwa uchambuzi kulinganishwa na matamko 7,732 mwaka 2019/20.

"Dosari zingine kwenye matamko ni kutotoa taarifa za wenza hasa taarifa za fedha zilizoko benki, kutokujaza baadhi ya vipengele muhimu, kutotamka thamani ya mali, kutoanisha na kushindwa kutoa ufafanuzi wa vyanzo vya mapato yao," alisema Jaji mstaafu Mwangesi.

# Msigwa, Sugu wachuana kwa hoja

**Na Elizabeth Zaya**

WAGOMBEA wa Uenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa na Joseph Mbilinyi 'Sugu' wameanza kuchuana kwa hoja nzito:

Sugu amedai amejitosa kwenye nafasi hiyo kutokana na msukumo wa wanachama ambao hawaridhishwi na uongozi wa sasa na hivyo kutaka mabadiliko.

Mch. Msigwa amesema hoja hiyo haina mashiko kwa kuwa kanda hiyo ndiyo inaongoza kwa kuandikisha wanachama wake kidigiti. Kama ingekuwa na migogoro, hilo lisingewezekana.

Mch. Msigwa anatetea nafasi yake kwa mara nyingine wakati Sugu ni mara ya kwanza kuingia kwenye kinyang`anyiro hicho.

Juzi wagombea hao walikutanishwa uso kwa uso katika mdahalo uliorushwa kupitia kipindi cha 'Medani za Siasa' cha kituo cha runinga cha Star Tv.

Sugu alisema aliamua kujitosa kwenye nafasi hiyo si kutokana na kuangalia mabaya au mazuri aliyoyafanya Mc. Msigwa bali vurugu za wanachama wenyewe ambao hawaridhishwi na mpinzani wake huyo wa sasa na hivyo kutaka mabadiliko.

Alimrushia lawama Mch. Msigwa kwamba ameshindwa kutatua migogoro iliyopo katika kanda hiyo, kutumia vibaya Katiba ya chama kuhalalisha mambo yake, kutengeneza vijana kuwa 'machawa' wake na kushindwa kujenga ofisi ya chama.

"Mimi nikichaguliwa, nitakuwa mwenyekiti wa kuleta umoja na kuweka watu pamoja, ili tuwe na CHADEMA Kanda ya Nyasa salama ambayo haina migogoro kama ilivyokuwa sasa hivi," Sugu alisema.

Naye Mch. Msigwa alijibu kwa kuhoji kwanini kanda hiyo iongoze kwa wanachama wake kujiandikisha kidigiti kama kweli ina migogoro anayoisema Sugu.

Alisema akichaguliwa kwa mara nyingine, atakuja kwa kasi kubwa zaidi kwa kutumia uzoefu wake aliopata katika kipindi chote akiwa kwenye nafasi hiyo.

"Nitakuwa mwenyekiti wa kuunganisha wanachama, kuongeza shauku, ari na hamu ya wanachama kukipenda chama chao zaidi, kukabiliana na CCM ambayo ndio mahasimu wetu kisiasa. Wanachama na wapenzi wa Kanda ya Nyasa wategemee kumpata Msigwa anayekuja kwa kasi kubwa zaidi," alisema Msigwa.

Alisema anaiona Nyasa kama jiwe la dhahabu ambalo ni tunu ya chama chao kukabiliana na CCM, hivyo wanahitaji kiongozi mwenye maono ya kuunganisha watu na anayefundisha.

Kuhusu migogoro kwenye kanda yake, Mch. Msigwa alisema, "Mwarobaini huwa hautupiwi mawe, unaotupiwa mawe ni mwembe, kwenye chama chetu tuna kanda 10, kwenye kanda hiyo, Nyasa inayoitwa ya migogoro ndiyo kinara wa kanda zote, sisi tumesajili wanachama wengi zaidi, migogoro yote inayojitokeza huwa tunaitatua kwa kuzingatia Katiba ya chama."

Kuhusu rushwa, Mch. Msigwa alisema haamini katika kutumia rushwa kupata uongozi, hahitaji kununua uongozi kwa sababu hata akikosa uongozi hatakufa.

Kwa mujibu wa CHADEMA, baada ya kufanyika uchaguzi katika Kanda ya Victoria juzi, uchaguzi mwingine katika kanda tatu za Nyasa, Serengeti na Magharibi utafanyika Mei 29 mwaka huu.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Mkakati wawekwa kunasa wakopeshaji mikopo umiza

**Na Josephine Majula,** MISSENYI

WANANCHI wilayani Missenyi, mkoani Kagera wametakiwa kufichua wamiliki wa taasisi za kukopesha fedha zisizo rasmi ili serikali ichukue hatua kali dhidi yao na kuzuia wengi kuumizwa na mikopo isiyofuata taratibu za kisheria.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Missenyi, John Wanga, ambaye aliambatana na timu ya wataalamu wa Wizara ya Fedha wanaoendelea kutoa elimu ya fedha kwa wananchi mkoani Kagera.

Tayari timu hiyo imetembelea wilaya nne za mkoa huo ambazo ni Bukoba, Missenyi, Muleba na Biharamulo ambako ilifanya mikutano ya kuelimisha wananchi namna ya kutambua wakopeshaji halali na hatua wanazotakiwa kuchukua wanapokutana na mkopeshaji ambaye hafuati matakwa ya kisheria.

"Sisi viongozi wa serikali tunatakiwa tuendelee kushirikiana na wananchi kuwakemea watoa huduma wasio na nia njema kwa taifa wanaojali maslahi yao binafsi huku wakiwaumiza wananchi," alisema Wanga.

Alisema serikali haitasita kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika kwenda kinyume cha maelekezo waliyopewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kabla hawajapatiwa leseni ya kuendesha shughuli za utoaji mikopo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Flavian Nturwa, alisema ni wajibu wa waratibu wote wa huduma ndogo za fedha kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi katika ngazi zote ili wawe na uelewa mpana wa masuala ya fedha.

"Tutahakikisha tunafanya mikutano ya mara kwa mara kwa wananchi wa pande zote, watoa mikopo na wapokeaji, ili wawe na uelewa wa pamoja hususan elimu ya mikataba kuepuka kusaini mikataba yenye masharti magumu," alisema Nturwa.

Mtoa Huduma za Mikopo, Salehe Hamisi alisema elimu itolewe juu ya utaratibu wa kusajili taasisi za fedha ili wafanyabiashara wajisajili kwa wingi na kutambulika rasmi.

Ofisa Usimamizi wa Fedha Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Mary Mihigo, alisema ni muhimu kila mmoja kuwa na nidhamu ya fedha ili kufikia malengo na kurejesha mkopo aliochukua.



Wizara ya Fedha inaendelea kutoa elimu juu ya huduma ndogo za fedha ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na elimu ya huduma ndogo za fedha kuepuka 'mikopo umiza'.

# Wananchi kukopeshwa bil. 10/- kupitia simu

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI milioni moja wanatarajiwa kuwezeshwa mikopo ya zaidi ya Sh. bilioni 10 kupitia simu zao.

Hatua hiyo inatokana na Benki ya CRDB kuingia makubaliano na kampuni ya mawasiliano ya Tigo Tanzania kuwezesha wateja wa Tigopesa wanaokidhi vigezo vya kukopa kuanzia Sh. 500,000 mpaka milioni mbili kufanya hivyo kupitia huduma ya Tigo Nivushe iliyoboreshwa.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema makubaliano hayo yanalenga kuwezesha Watanzania kupata mkopo utakaowasaidia kufanikisha shughuli zao mahali popote walipo, hivyo kuchangia kasi ya kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa taifa kwa ujumla.

"Benki ya CRDB inatarajia kuhudumia wateja wa Tigo Nivushe wanaokidhi vigezo vya kukuwawezesha kupata mikopo ya kuanzia Sh. 500,000 mpaka Sh. milioni mbili. Kwa miaka mitatu ijayo, tunatarajia kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili yao na kupata wateja zaidi ya milioni moja," alisema Nsekela.

Mkataba huo, Nsekela alisema umetiwa saini baada ya kufanya majaribio kwa miezi mitatu na kuwafikia takriban wateja 100,000, hivyo pande zote mbili kujiridhisha kwamba zipo tayari kuanza kuwanufaisha Watanzania wenye uhitaji na fedha kwa matumizi tofauti.

Mkurugenzi huyo alisema wanafahamu ukubwa wa uhitaji wa mikopo nafuu walionao wananchi hasa wale ambao hawatumii huduma za benki, hivyo wanashirikiana na kila mdau anayeweza kusaidia kuwafikia wananchi na kampuni ya Tigo ni miongoni mwa taasisi walizoona ni sahihi kufanikisha lengo hilo.

Kwa sasa, serikali inatekeleza Mpango Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa Mwaka 2023 - 2028 chini ya Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha ili uendeleza mafanikio yaliyopatikana katika mkakati wa pili ikiwamo ongezeko la watu wazima wanaotumia huduma rasmi za fedha nao wakiongezeka kutoka asilimia 65 mwaka 2017 hadi asilimia 76 mwaka 2023.

Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoTO inasema mafanikio haya yanaelezwa kuchangiwa zaidi na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za fedha kwa njia ya kidijitali, uelewa wa huduma za fedha kwa watumiaji, na ushirikiano kati ya wadau wa huduma jumuishi za fedha wa sekta ya umma na binafsi.

Katika Mpango huu wa Tatu, dira ya serikali ni kuona rika la watu wazima na wafanyabiashara wote wanafikiwa na kutumia bidhaa na huduma bora za fedha ili kuboresha ustawi wa maisha yao ya kila siku kwa kuishirikisha binafsi pamoja na wadau wa maendeleo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tigopesa, Angelica Pesha alisema teknolojia imerahisisha kila kitu na idadi ya Watanzania wanaotumia simu za mkononi ambazo ni njia nzuri ya kuwafikishia huduma za fedha inazidi kuongezeka kia siku.

"Takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaonesha kuna takriban akaunti milioni 53 za pesa mtandao. Kati ya hizo, akaunti milioni 16.5 ni za Tigopesa. Hawa ni Watanzania waliopo mjini na vijijini, hivyo ushirikiano huu tunaoanza leo na Benki ya CRDB utafika katika kila pembe ya nchi yetu kuwanufaisha wananchi," alisema Angelica.

Katika utoaji huduma kupitia simu za mkononi, Angelica amesema wanao uzoefu wa kutosha, hivyo wanapoungana na Benki ye CRDB ambayo ni taasisi kubwa zaidi ya fedha nchini, wanalenga kuacha alama kwa Watanzania wengi ambao sasa hawatopoteza muda wala kutafuta wadhamini kupata mkopo wa mpaka Sh. milioni mbili.

"Huko mtaani kuna masharti mengi ya kukopa Sh. milioni mbili. Utatakiwa uwe na wadhamini pamoja na dhamana lakini sisi Tigo na Benki ya CRDB tumeungana kurahisisha na kuondoa usumbufu huo wote ambapo sasa hivi mtu ataweza kupata fedha anayoihitaji kwenye simu yake," alisema Angelica.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...30/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MOHAMED OMARY MAFIGA wa MJIMPYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA SEMMY JUMA OMARY**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 5 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 5 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO
HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...30/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MOHAMED OMARY MAFIGA wa MJIMPYA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA SEMMY JUMA OMARY**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 5 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 5 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO
HAKIMU

## Katibu CCM ahadharisha NGO zinazoisemea serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU wa Siasa, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani, David Mramba, amesema mashirika yanayoanzishwa kwa ajili ya kuisema serikali na kuhakikisha hayatumiki kama kichaka cha maovu.

Mramba alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokutanisha mashirika yasiyo ya kiserikali yenye mrengo mmoja wa kuisemea CCM na serikali, akisisitiza "wanapaswa kuwa wazalendo wa kweli".

Katibu huyo alisema yapo baadhi ya mashirika yamegeuka kichaka cha kuhifadhi uovu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha malengo ya uanzishwaji na kuchafua serikali na chama tawala, jambo ambalo halipendezi kwa jamii.

Mramba pia alisema ni muhimu mashirika hayo kufanya kazi kwa manufaa ya taifa na si kujinufaisha huku akionya wanaojiingiza kwenye migogoro ya wagombea wa nafasi mbalimbali katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025.

"Fanyeni kazi za taasisi zenu kwa bidii na kuepuka ubadhirifu mkizingatia lengo la kuanzishwa kwake, msiingie kwenye taasisi kufuata uteuzi," alisema Mramba.

Katibu huyo alisema ni muhimu kufuata taratibu za kisheria kwa kusajiliwa ifikapo Juni mwaka huu ili watambulike kwa mujibu wa sheria za nchi na kuheshimu taratibu zilizowekwa.

Katibu wa Siasa, Uenezi na Mafunzo wa CCM Mkoa wa Morogoro, Zagina Shanang, alikumbusha wanachama wa chama hicho kuhakikisha katika uchaguzi ujao wanachagua viongozi ambao wana shughuli za kuwaingizia kipato.

Shanang pia alionya mashirika hayo dhidi ya tabia za ubaguzi na kutengeneza makundi ya wagombea huku akisisitiza wanawake kupewa nafasi zaidi za uongozi.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo ulioambatana na mafunzo, Mohamed Mzimba, alimpongeza Katibu wa Siasa Uenezi na Mafunzo kwa kukutanisha mashirika hayo na kujadili kwa pamoja mambo ya kukijenga chama na taifa kwa ujumla.

# Wataka Waziri wa Fedha apunguziwe mamlaka, Bunge limulike mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa masuala ya madeni na maendeleo wameshauri serikali kushirikisha Bunge kabla ya kukopa ili kuondoa uwezekano wa mikopo kuishia mifukoni mwa watu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD), Hebron Mwakagenda, alitoa ushauri huo juzi wakati wa mkutano wa kitaifa wa madeni na maendeleo wenye lengo la kujadili mwenendo wa Deni la Taifa.

Mwakagenda alisema wanashauri badala ya Waziri wa Fedha kupewa mamlaka ya kukopa kama ilivyo sasa, utaratibu huo ubadilishwe, Bunge liwe na uwezo wa kupitia kila mkopo wa serikali na kujiridhisha kama una tija na taifa.

"Sisi tunatamani Bunge kushirikishwa kwenye mchakato wa ukopaji mikopo ya serikali badala ya mamlaka hayo kupewa Waziri wa Fedha pekee yake.

"Kuwapo utaratibu kama serikali inataka kukopa, basi ombi hilo la mkopo kwanza lipitiwe na kamati husika ya Bunge, kwani huko ndiko kwenye uwakilishi wa wananchi, hali hii pia itasaidia kuondoa uwezekano wa mikopo kuishia mifukoni mwa watu," alisema.

Mwakagenda alisema zipo baadhi ya nchi Afrika ambazo fedha za mikopo zilikopwa na huishia mifukoni mwa watu.

"Lakini kama Bunge litashirikishwa na kuwa na wataalamu huru ambao watapitia maombi ya mikopo kutoka kwa Waziri wa Fedha basi mikopo itakayokopwa itakwenda kwenye miradi iliyokusudiwa na si vinginevyo.

"Kamati ya Bunge itakuwa na uwezo wa kumhoji waziri, mkopo ni kwa ajili ya kitu gani na itasaidia kukopa tu pale ambapo kuna uhitaji na ulazima lakini tukikopa lazima tuhakikishe deni linalipwa," alisema.

Aliongeza kuwa hivi sasa nchi nyingi za Afrika zimeingia kwenye mzigo wa madeni makubwa kutokana na kukopa pasi na kuwajibika.

Alisema nchi za Afrika zinapaswa kubadilika ili kuondokana na mzigo wa ukuaji Deni la Taifa, hali inayosababisha serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha kuhudumia deni na kusababisha baadhi ya miradi ya maendeleo kushindwa kutekelezwa.

"Tunapaswa kukopa kwa uwajibikaji, tukope pale tu kwenye ulazima, tukope kwa kuangalia kizazi kijacho kwani tunaweza kukopa leo lakini mzigo tukawaachia watoto wetu.

"Hivi karibuni wakati wa maadhimisho ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan, mwenyewe alisema tumekopa sana na kushauri kuwa tupunguze kasi na sisi kama wadau wa masuala haya ya madeni na maendeleo tulifurahia sana kusikia ile kauli," alisema.

Mwakagenda alisema serikali inapaswa kujiimarisha kwenye ukusanyaji mapato ili kuwa na uwezo wa kulipa madeni yote inayokopa badala ya kukopa sehemu ili kulipa sehemu nyingine.

"Wenzetu Uganda uwanja wao wa ndege umechukuliwa kulipa deni, Zambia shirika lao la umeme limechukuliwa kufidia deni, hivyo tujiandae, hizi ndizo athari za kukua kwa Deni la Taifa," alisema Mwakagenda.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inaonesha katika kipindi cha mwaka 2022/23, Deni la Serikali liliongezeka kwa asilimia 15 na kufikia Sh. trilioni 82.25 huku serikali ikisisitiza kuwa bado ni himilivu.

# Mbunge ataka wanahabari kutumia kalamu zao vizuri

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood amehimiza waandishi wa habari kutumia kalamu zao kuandika masuala yatakayoleta matokea chanya nchini pamoja na kazi zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kimkoa yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari, mkoani Morogoro (MOROPC), Abood alisema mwishoni mwa wiki kuwa wanahabari wana nafasi kubwa kuhamasisha masuala mbalimbali ya kimaendeleo ili kuunga serikali mkono katika kuletea maendeleo wananchi.

Alisema Rais Samia anafanya kazi kubwa kuwaletea maendeleo wananchi kwenye sekta ya afya, elimu, barabara na maji lakini baadhi ya watu wanabeza utendaji kazi wake.

Alisema wanahabari wana kila sababu ya kuhabarisha umma kuwaeleza kila kinachofanywa na serikali hasa katika kuwahudumia wananchi ili watu wenye nia mbaya na serikali wasipate nafasi ya kusambaza uongo.

Alitolea mfano kwa Jimbo la Morogoro Mjini, limepokea fedha nyingi kutoka serikali kuu na kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo kuna kila sababu ya kumshukuru Rais Samia hususani ujenzi wa miradi ya maji, hospitali na zahanati na miundombinu mingine ya barabara.

Abood alisema serikali inathamini kazi nzuri inayofanywa na wanahabari katika kutangaza mafanikio ya serikali na changamoto za jamii hivyo itaendelea kutoa ushirikiano katika utendaji kazi wao.

Abood ambaye ni Mlezi wa MOROPC, alisema ataendelea kushirikiana na vyombo vya habari katika kuleta maendeleo.

Mwenyekiti wa MOROPC, Nickson Mkilanya, alisema chama hicho kimeadhimisha kwa kupanda miti katika Mto Lukulunge ambao unachangia maji Bwawa la Mindu.

Alisema hatua hiyo inatokana na kuwapo mabadiliko ya tabianchi yaliyoleta athari kubwa nchini hivyo wanahabari wanatakiwa kuunga mkono kwa vitendo mapambano ya uharibifu wa vyanzo vya maji.

Mkilanya aliahidi MOROPC itaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na uharibifu wa mazingira pamoja na kuchochea matumizi ya nishati safi na salama.

# Wadau 2,240 wamchangia Lissu mil. 25/- anunue gari

**Na Jenifer Gilla**

MCHANGO wa fedha za kumnunulia gari Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu umefikia Sh. milioni 24.9 ndani ya siku saba tangu kuanzishwa kwa harambee hiyo.

Lissu alithibitisha kupokea kiasi hicho cha fedha kupitia mtandao wake wa X juzi na kuomba wadau waendelee kumchangia apate gari hilo "kwa ajili ya harakati za ukombozi".

Mei 17 mwaka huu, wafuasi wa mwanasiasa huyo wakiongozwa na Mwanaharaki Maria Sarungi, waliazimia kumchangia fedha mwanasiasa huyo anunue gari jipya ili lile la zamani ambalo lilishambuliwa kwa risasi lihifadhiwe kwa ajili ya ukumbusho.

"Tumekamilisha wiki moja ya mchango. Hadi sasa tumepokea Sh. 24,956,282.00 kutoka kwa wachangiaji 2,243. Kwa wastani, kila siku wachangiaji 320 wametoa Sh. 11,126.30 kila mmoja," aliandika Lissu kwenye ukurasa wake wa X.

Wiki iliyopita Lissu alikabidhiwa gari lake aina ya Toyota Land Cruizer V8, VXR na Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, ikiwa iimepita takriban miaka saba tangu aliposhambuliwa na watu wasiojulikana nyumbani kwake Area D, jijini Dodoma Septemba 7, 2017.

Baada ya kukabidhiwa gari hilo, Lissu alieleza lengo lake la kulitengeneza gari hilo ili kulitumia kwenye shughuli za kisiasa, jambo ambalo lilipingwa na wafuasi wake wakisisitiza watamnunulia gari jipya. Hilo liwekwe Makumbusho ya Taifa ili vizazi vijavyo vione yaliyotokea.

Ndani ya saa 48 tangu Maria kuweka namba za malipo kwa ajili ya kukusanya fedha hizo kupitia mitandao ya kijamii ya X na Instagram zilikusanywa Sh. milioni 15.

Lengo la mchango huo ni kuhakikisha ndani ya mwezi mmoja kinapatikana kiasi cha fedha kitakachotosheleza kununua gari linalofanana na lililoshambuliwa kwa risasi ili Lissu aendelee na shughuli zake za kisiasa.

Katika ukurasa wake wa X, Maria juzi aliendelea kuhamasisha wafuasi na wapenzi wa kiongozi huyo kuchanga ili kiasi hicho cha fedha kipatikane na gari linunuliwe kwa muda waliopanga.

"Tukishikamana tunaweza, kuhamasishana kila mtu unayemjua atoe Sh. 1,000 au 500, tukiamua watu 10,000 kutoa Sh. 1,000 kwa siku tunapata milioni 10 ndani ya mwezi tunamalizia kilichobaki," aliandika Maria kwenye ukurasa wake wa X.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE
CPP
BR SUNMAKER

## Call Applications for SMAW Welding Training

CHINA PETROLEUM PIPELINE ENGINEERING CO, LTD is a contractor for Pipeline of East African Crude Oil Pipeline (EACOP) Project. Sunmaker Development and Consulting (Tanzania) Limited is contracted by CHINA PETROLEUM PIPELINE ENGINEERING CO, LTD to undertake:

1. **Shielded Metal Arc Welding (SMAW) - Welding Training**

The individual originating candidates will be covering the whole Tanzania nationally.

**Eligibility / Requirements:**

- Must be above 18 years of age
- An individual needs to understand the working environment very well and be able to adapt smoothly to various working situations.
- Individuals must hold National Vocational Awards/Vocational Certificates Levels I or II or III in Welding and Metal Fabrication / Auto Body Repair / Fitter Mechanics / Fitter Turner / Auto Body Repair / Boiler Mechanics / Plumbing / Pipe Fittings.
- Successful applicants should be ready to stay at the training Institute for at least 280 training hours to complete the training.

**Physical Requirements:**

- Eyesight Test; This will be tested by the Selecting Officers using Optotype. Minimum requirement is <= -1.0D.
- Steady Hands and Good Hand-Eye Coordination
- Ability to be able to perform all essential functions required; Sit, climb, see, balance, hear, walk, smell, talk, reach, stand, stoop, kneel, crouch, and crawl. This will be tested by the Selecting Officers during Interviews.
- Colour Blind Test; This will be tested by the Selecting Officers during Interviews.
- Vision test Jaeger N°1 @ 30cm; Ability to read J1 without squirting

**Knowledge Requirements:**

- Ability to spot a dangerous environment and implement procedures to prevent illness or accidents, as well as circumstances that might negatively affect morale or mental health. This will be tested by the Selecting Officers during Interviews using specific tools/instruments.
- Strong critical thinking skills, Ability to practice and maintain active listening, problems solving, Team management Ability to articulate and communicate well with others. This will be tested by the Selecting Officers during Interviews using specific tools/instruments.

**Application Procedure:**

- Interested candidates should get the Application Forms from the designated offices/locations in the districts as indicated below. Or email your CV to nadjakabati@brpetro.com.
- Fully completed application forms with supporting documents attached should be returned to the designated offices/locations where the forms were collected before the deadline date mentioned below.

**Physical Interviews will be conducted at:** **Arusha Technical College (ATC)**

- After completing the application form, return it with supporting documents; National ID Card Copy, Latest Education Certificate and all previous education certificates, Passport size Picture, Previous experience (if available) etc., to the place where you picked it from in a sealed envelope.
- After screening process, online interview is available to candidates who can not make it to Arusha. A Link to **Teams Meeting App** will be provided via email.
- The trainee who has passed the test upon completion will be given priority/preference to sign an employment contract with CHINA PETROLEUM PIPELINE ENGINEERING CO, LTD. And the trainee should sign the contract and commit to providing services for CHINA PETROLEUM PIPELINE ENGINEERING CO, LTD for at least two years starting from the contract signing date.

**Deadline:**

- The deadline for submission is **19th June 2024 at 5 PM**. Any application form submitted after that time shall not be considered for evaluation to join the training program.

**Contacts:**

- For information Candidate will be contacted via email nadjakabati@brpetro.com.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msimu umeisha, maandalizi sasa yaanze 2024/25

**YANGA** imetangazwa kuwa bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2023/24, mechi za mwisho zikitarajiwa kuchezwa kesho.

Ubingwa huo wa Yanga ni wa tatu mfululizo ikiipokea Simba iliyotoka kutwaa mara nne mfululizo kuanzia msimu wa 2017/18 mpaka msimu wa 2020/21.

Kutangazwa kwa Yanga kuwa mabingwa kunaashiria msimu wa ligi hiyo kufika mwishoni na sasa inachezwa michezo ya kukamilisha ratiba.

Kumalizika kwa msimu wa ligi kunaashiria kuanza maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Agosti mwaka huu kwa timu zilizobaki na zile zilizopanda daraja msimu huu.

Klabu ambazo zimepata bahati ya kupanda daraja na zile zilizobakia Ligi Kuu zianze sasa kujipanga kwa kwa ajili ya msimu ujao wa ligi hiyo.

Ubingwa wa Yanga au kufanya vizuri kwa klabu ya Azam FC havikuja kwa bahati, ni mipango na mikakati iliyowekwa na viongozi wa klabu hizo.

Kwa sasa mashabiki na wanachama wa Yanga wanatembea kifua mbele wakitamba kutokana na mafanikio ya timu yao.

Kwenye kila mafanikio kuna juhudi zilizofanywa. Ubingwa wa Yanga wa tatu mfululizo umetokana na juhudi za viongozi wake kuwekeza na kutengeneza kikosi bora.

Kumalizika kwa msimu huu sasa kunatoa fursa kwa klabu zingine kujiandaa kwa msimu ujao wa ligi uliopangwa kuanza miezi mitatu ijayo.

Kujiandaa ni pamoja na kuwa na benchi zuri la ufundi, kusajili wachezaji wazuri na wenye ubora pamoja na kufanya maandalizi mazuri kwa kikosi kizima.

Kengold FC na Pamba FC ni timu mpya Ligi Kuu msimu ujao, zinapaswa kujipanga vizuri ili kutoa ushindani wa kweli na kuendelea kusalia kwenye ligi hiyo.

Pamba FC imetumia zaidi ya miaka 20 kurejea tena Ligi Kuu, inapaswa kujipanga na kujiandaa vyema ili kuendelea kusalia kwenye ligi hiyo, vinginevyo irejee ilikokuwa.

Kwa timu ambazo zimebakia msimu huu wa Ligi Kuu na zilikuwa kwenye hali mbaya, ni wakati mwafaka kwao kujipanga upya kwa kuandaa timu nzuri kwa ajili ya ushindani msimu ujao.

Mtibwa Sugar, moja ya timu 'king'ang'anizi' kwenye Ligi Kuu, iliyotwaa ubingwa mwaka 1999 na 2000 na haikuwahi kuporomoka daraja tangu ilipopanda Ligi Kuu, msimu huu imeshuhudiwa inashuka daraja na kwenda kucheza 'Championship'. Hili halijatokea isivyo bahati.

Matokeo mabaya waliyokuwa wanapata kwenye mechi zao yamesababisha kushuka daraja. Ni funzo kwa timu nyingine kuhakikisha zinakuwa na timu nzuri ili kutoa ushindani.

Mtibwa ni kama chuo cha soka kwa wachezaji wazawa, wachezaji wengi wanaowika sasa wamepitia kwenye timu hiyo inayosifika kwa kutoa nafasi kwa vijana kuonesha vipaji vyao.

Tunataka kuona msimu ujao unakuwa na ushindani zaidi ya msimu huu, kila timu ijiandae na kujipanga, ifanye usajili mzuri na wenye tija kwa maendeleo ya timu.

Tunakumbusha klabu, ligi imemalizika na sasa zijipange kwa ajili ya msimu ujao, zisajili vizuri ili kuendelea kuiongeza thamani ligi yetu inayotajwa kuwa namba tano kwa ubora barani Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Yanga ilistahili ubingwa, timu zijipange msimu ujao

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu 2023/24 imeisha ikishuhudiwa Yanga ikitwaa ubingwa msimu huu, ikiwa ni mara ya tatu mfululizo.

Msimu huu umeshuhudiwa anguko la timu ya Simba ambalo hata ushindi wa pili tu kwake inautafuta kwa shida ambapo hatima yake ni kesho itakapocheza dhidi ya JKT Tanzania.

Ili kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao, Simba inahitajika kushinda zaidi ya mabao manane kwenye mechi hiyo, au kuiombea Azam FC ifungwe au walau tu kutoka sare dhidi ya Geita Gold.

Matokeo yoyote kinyume cha hapo yataitupa Simba kwenye Kombe la Shirikisho na kukosa kucheza Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza baada ya misimu sita kupita.

Pamoja na matatizo na mapungufu ya hapa na pale, Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), Bodi ya Ligi, pamoja na Kamati ya Waamuzi, wamejitahidi kuisimamia kwa kadri wanavyoweza ili kila timu kupata haki yake.

Japo si kwa asilimia zote, lakini timu nyingi zimetendewa haki, kiasi kwamba ilikuwa ni ngumu kutabiri timu yoyote kama inaweza kushinda hata nyumbani.

Kumekuwa na mechi nyingi zaidi ambazo timu zimeshinda ugenini, ndiyo maana uliona msimu huu baadhi ya timu hata zile zinazoitwa au kujiita ndogo zikitamba kwenye kushinda nje ya uwanja wao wa nyumbani.

Nitoe hongera kwa Yanga kwa kutwaa ubingwa msimu huu, kwa sababu ilionekana kujipanga mapema, ndani na nje ya uwanja.

Ilitengeneza uongozi imara uliokuwa inasimamia kile ambacho imekipanga na kukitekeleza.

Ilifanya usajili si mkubwa, ila ni wa maana, uliokuwa kwenye mahitaji muhimu na wachezaji wenye ubora, bila kujali gharama.

Ilitengeneza benchi la ufundi bora, ambalo lilisimamia ufundi na utimamu wa mwili wa wachezaji.

Ndiyo maana hata kama wachezaji muhimu wa Yanga hawapo, waliobaki ambao hawachezi siku zote waliokuwa na uwezo wa kuamua mechi.

Ukiwaangalia wachezaji wa Yanga, hata kama hawana ubora mkubwa, lakini utimamu wao wa mwili uliwasaidia sana.

Uongozi ulisimamia nidhamu, miiko na maadili ya mpira wa miguu na klabu hiyo kwa ujumla, mwisho wa siku ikawalipa.

Simba msimu huu iliathiriwa na usajili mbovu iliokuwa inaufanya kwa madirisha sita ya usajili kwa misimu mitatu, ikitegemea kubebwa kwa kiasi kikubwa na wachezaji wale wale wa miaka nenda rudi ambao kwa sasa viwango vyao vimeporomoka kwa kasi kubwa kutokana ya umri wao mkubwa, kucheza misimu yote mfululizo bila kupumzika, au kutokuwa na chochote cha kuongeza kwani tayari wengi wao walishaipa timu ubingwa mara nne na robo fainali tano za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ndani ya kambi ya Simba inaonekana kama wachezaji wana nguvu zaidi kuliko viongozi, kwa sababu umeripotiwa utovu mkubwa wa nidhamu wachezaji wengi wakitoroka, lakini wamekuwa hawafanywi kitu.

Wachezaji wa Simba hata ukiwaangalia wanapocheza, hawana utimamu wa mwili, hii imewafanya washindwe kumiliki mpira kwa muda mrefu wapocheza na wapinzani wao.

Ifike mahali viongozi wa Simba waangalie kwa jicho lingine safari za kwenda nje ya nchi kama vile Uturuki, Morocco au Oman, kuweka kambi ya mwanzo wa msimu kwani zimeonekana haziwasaidii, badala yake timu msimu mzima inakosa stamina.

Na hii inasababisha wanatumia muda mrefu kuwasafirisha wachezaji, wakisafiri mafungu mafungu, wengine wakiwa hawajakamilisha usajili, wanapokuja yale mazoezi ya 'pre seasons' yanakuwa yameshakamilika.

Nadhani kuna kitu watakuwa wamejifunza, ni bora kukaa hapa hapa na kuwapa wachezaji mazoezi mazito ya mwanzo wa msimu ili wawe na stamina na pumzi.

Hongera pia kwa Azam FC, ambayo msimu huu imetoa ushindani mwanzo mpaka mwisho wa ligi, tofauti na msimu kadhaa iliyopita ilipokuwa ikitupa taulo mapema.

Hongera pia kwa Coastal Union kwa kukata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho kwani mwanzo wa msimu haikudhaniwa kama inaweza kufanya hivyo. Ila ijipange si na michuano hiyo migumu, bali hata na gharama za uendeshaji na usafiri.

Mtibwa Sugar ambayo imeshuka daraja nayo ni haki yake, kwani haikujifunza misimu mitatu iliyopita ilipokuwa ikiponea katika mechi za mchujo 'Play Off'.

# RC: Wafanyabiashara ipeni ushirikiano TRA

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Dk. Batilda Buriani, amewataka wafanyabiashara kutoa ushirikiano kwa timu ya uelimishaji kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Timu hiyo inaendelea kutoa elimu ya kodi mlango kwa mlango kwa wafanyabiashara kwa kuwatembelea katika maeneo yao ya biashara.

Dk. Batilda ameomba wafanyabiashara wafunguke kwa TRA ili wasikilizwe na kutatuliwa changamoto zao za kikodi huku akisisitiza matumizi sahihi ya risiti za kielektroniki (EFD) kwa wafanyabiashara kuhakikisha wanatoa risiti halali kila wanapofanya mauzo na wanunuzi kudai risiti sahihi kila wanapofanya ununuzi.

Aliekeleza hayo mwishoni mwa wiki alipotembelewa na timu ya uelimishaji ya TRA ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano TRA, Hudson Kamoga kwa lengo la kumpa maelezo juu ya zoezi zima la elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango na kliniki za kodi linaloendelea mkoani Tanga.

"Kodi kwa maendeleo ya taifa letu. Tukumbuke kwamba kodi ndiyo inasaidia kutekeleza miradi ya bandari, barabara zetu. Haitafurahi kuona makusanyo yetu ya kodi ni madogo ilhali uwezo wetu wa kukusanya kodi ni mkubwa.

"Kila Mtanzania, kila mwananchi wa Tanga, kila ukienda dukani au mahali popote kununua bidhaa au huduma, dai risiti, wewe muuzaji toa risiti kila unapouza.

"Wenzetu hawa wa TRA wamekuja kupatia elimu, tuwape ushirikiano. Hakuna matumizi ya mabavu, tuhakikishe kodi inakusanywa vizuri ili tupate maendeleo," alisema Dk. Batilda.

Kaimu Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano TRA, Kamoga aliwaomba wafanyabiashara kutoa ushirikiano wakati wa zoezi hilo.

Alielekeza wenye changamoto zozote za kikodi na wanaohitaji huduma TRA wasisite kuhudhuria kliniki za kodi zitakazokuwa mtaani kwao kwa ajili ya kuwahudumia wafanyabiashara.

TRA imekuwa inaendesha kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango kwa kutembelea wafanyabiashara katika maeneo yao ya biashara na kuwapa elimu ya kodi.

Kampeni hiyo inatajwa na TRA kuwa na manufaa makubwa kwa kuongeza ulipaji kodi wa hiari na sasa timu ya uelimishaji iko Tanga kwa siku 10 kuanzia Mei 20 mwaka huu ikitoa elimu ya kodi mlango kwa mlango na kuendesha kliniki za kodi.

# Jela miaka 30 kwa kuiba simu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Ndoro, Manispaa ya Lindi, Naibu Ally (20), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kukutwa na hatia ya kupora kwa kutumia panga simu aina ya Tecno 8 yenye thamani ya Sh. 667,000, mali ya Husna Bilali.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Conslatta Singano, baada ya kuridhishwa pasi na shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kama anazo sababu za msingi ili mahakama isimpe adhabu kali, naye aliendelea kudai hahusiki na wizi huo, bali anasingiziwa.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Singano alimwuliza Wakili wa Serikali Hilali Kabyemela, kama anazo kumbukumbu za makosa ya zamani ya mshtakiwa, naye alijibu kwa kudai ni mhalifu sugu, ana kesi zingine katika mahakama ya mwanzo na kuomba mahakama kumpa adhabu kali iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia za aina hiyo.

Hakimu Singano alirejea kifungu 287 (4) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, marejeo ya 2022, akamhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

"Mshtakiwa kama hujaridhika na hukumu uliyopewa, milango ya kukata rufani iko wazi," alisema Hakimu Singano.

Awali ilidaiwa mahakamani huko na Wakili wa Serikali Kabyemela kwamba mshtakiwa akiwa na wenzake wawili, Salum Kambi (24) na Athumani Lwanda (24) ambao wameachiwa huru kutokana na ushahidi kutowatia hatiani, wakiwa na silaha aina ya panga, walimpora mlalamikaji simu yake aina ya Tecno 8 yenye thamani ya Sh. 667,000 na kutokomea nayo.


## TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

### TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UZALISHAJI WA GESI YA HELIUM KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE

Gogota (Tz) Limited ambayo ni kampuni tanzu ya Helium One Global Limited inamiliki vitalu vya Leseni ya Utafutaji madini (PL) namba PL 10713/2015 chenye Kilomita za Mraba 297.58 na PL 10712/2015 chenye Kilomita za Mraba 264.25 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hii imekamilisha utafiti wa madini mwaka 2023 na imebaini uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10.

Kampuni ya Gogota (TZ) Limited, inatarajia kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA) kwa Mradi unaopendekezwa wa uzalishaji wa gesi ya helium kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni zake na sheria nyingine za Tanzania na Kimataifa. Eneo la Mradi liko katika Wilaya ya Momba ndani ya Mkoa wa Songwe.

Kanuni ya 17(2a) cha kanuni za udhibiti na ukaguzi wa athari za kimazingira ya mwaka 2005, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018, inamtaka muendeleza mradi kutoa taarifa kwa umma kuhusu mradi pendekezwa kwa muda wa wiki mbili mfululizo kwenye chombo cha habari ambacho kinasikika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathmini ya athari za uzalishaji wa gesi ya helium kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni ya Gogota (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu zitakazojumuisha vijiji tisa ambavyo ni Kamsamba, Muungano, Kasanu, Mpapa, Masanyita, Itumbula, Lwatwe, Samang'ombe na Mkonko.

Taarifa hii imetolewa kuomba maoni na mapendekezo ya wadau au pande zozote ambazo kwa namna moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mradi huu. Mtu yeyote mwenye maslahi, maoni, wazo au maarifa (ufahamu) kuhusu athari zozote za kimazingira na kijamii za mradi pendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anwani zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| **Mkurugenzi<br>Helium One (Gogota) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam, Tanzania<br>Mawasiliano: 0682 636 828<br>Barua pepe:gogota@helium-one.co.za** | **Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),<br>S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.<br>Mawasiliano: +255 22 2774889<br>Barua pepe:<br>nemc@nemctz.org** | **Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Limited,<br>Victoria House, Gorofa ya tisa, Kitalu Na. 37, Regent Estate, Barabara mpya ya Bagamoyo,<br>S.L.P 77894, Dar es Salaam.<br>Simu ya mezani: +255 22 2926117,<br>Simu ya mkononi:+255 767360225/743127611<br>Barua pepe: info@mtlconsultingtz.com** |



## TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

### TAARIFA YA AWALI YA MRADI TARAJIWA WA UZALISHAJI WA GESI YA HELIUM KATIKA WILAYA YA MOMBA, MKOA WA SONGWE

Njozi (Tz) Limited ambayo ni kampuni tanzu ya Helium One Global Limited inamiliki vitalu vya Leseni ya Utafutaji madini (PL) namba PL 10713/2015 chenye Kilomita za Mraba 297.58 na PL 10712/2015 chenye Kilomita za Mraba 264.25 katika eneo la mashariki mwa bonde la Rukwa, kusini mwa Tanzania. Kampuni hii imekamilisha utafiti wa madini mwaka 2023 na imebaini uwepo wa gesi ya Helium. Gesi hiyo inatarajiwa kuwa na kiwango cha kati ya asilimia 4.2 na 10.

Kampuni ya Njozi (TZ) Limited, inatarajia kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA) kwa Mradi unaopendekezwa wa uzalishaji wa gesi ya helium kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni zake na sheria nyingine za Tanzania na Kimataifa. Eneo la Mradi liko katika Wilaya ya Momba ndani ya Mkoa wa Songwe.

Kanuni ya 17(2a) cha kanuni za udhibiti na ukaguzi wa athari za kimazingira ya mwaka 2005, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018, inamtaka muendeleza mradi kutoa taarifa kwa umma kuhusu mradi pendekezwa kwa muda wa wiki mbili mfululizo kwenye chombo cha habari ambacho kinasikika nchi nzima. Kwa mantiki hiyo taarifa hii inawasilishwa kuufahamisha umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited imepewa kazi ya kufanya tathimini ya athari za uzalishaji wa gesi ya helium kwenye mazingira na jamii kwa niaba ya kampuni ya Njozi (TZ). Tathmini hii itafanyika katika kata tatu ambazo ni Mpapa, Ivuna na Kamsamba zitakazojumuisha vijiji vya Kipeta, Kilangawana, Kilyamatundu, Mkonko, Usoche, Mpapa, Mkuyu, Senga, Kamsamba, Itumbula, Samang'ombe, Lwatwe, Mpapa, Kasanu na Masanyita.

Taarifa hii imetolewa kuomba maoni na mapendekezo ya wadau au pande zozote ambazo kwa namna moja au nyingine wanaweza kuathiriwa na mradi huu. Mtu yeyote mwenye maslahi, maoni, wazo au maarifa (ufahamu) kuhusu athari zozote za kimazingira na kijamii za mradi pendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anwani zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| **Mkurugenzi<br>Helium One (Njozi) Limited.<br>Gorofa ya Pili, Kilwa House, 369 Toure Drive, Oyster Bay<br>S.L.P 62, Dar Es Salaam, Tanzania<br>Mawasiliano: 0682 636 828<br>Barua pepe:<br>njozi@helium-one.com** | **Mkurugenzi Mkuu,<br>Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),<br>S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.<br>Mawasiliano: +255 22 2774889<br>Barua pepe:<br>nemc@nemctz.org** | **Meneja Mkuu<br>MTL Consulting Limited,<br>Victoria House, Gorofa ya tisa, Kitalu Na. 37, Regent Estate, Barabara mpya ya Bagamoyo,<br>S.L.P 77894, Dar es Salaam.<br>Simu ya mezani: +255 22 2926117,<br>Simu ya mkononi: +255 767360225/743127611<br>Barua pepe: info@mtlconsultingtz.com** |

# UN yataja maeneo wanawake Tanzania wameachwa nyuma

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN-Women) limesema pamoja na kwamba asilimia 90 za ajira zote duniani kuegemea katika sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati, wanawake wameachwa nyuma nchini.

Limebainisha kuwa kwa Tanzania, kati ya wataalamu watano waliomo nchini kwenye taaluma ya sayansi, teknolojia na uhandisi, mmoja tu ni mwanamke (asilimia 20).

Mtaalamu wa Uchumi katika Mpango wa Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi wa UN-Women, Lilian Mwamdanga, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa kuadhimisha Wiki ya Ubunifu Tanzania 2024.

Lilian alipongeza Tanzania kwa jitihada na kujizatiti kwenye ubunifu na kutowaacha wanawake na wasichana, akisisitiza bado kunahitajika mabadiliko kimtazamo ili kuziba mgawanyiko kijinsia kidijitali.

"Kunahitajika kuboresha ufikiaji salama na rahisi, upatikanaji zana na ujuzi wa kidijiti ili kuhakikisha ushiriki kamili wa wanawake. Ubunifu ni miongoni mwa ajenda za Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na hii itaisaidia Tanzania kufikia matarajio yake ifikapo 2050," alisema.

Alisema ili kufanikisha hilo nchini, shirika hilo kupitia mradi wa 'African Girls Can Code-Binti Dijitali' Project, wanawake na wasichana walio na umri kati ya miaka 17 na 25 wanakuzwa vipaji katika taaluma hiyo na 100 wamepewa mafunzo.

"UN-Women inaendelea kujizatiti na kushirikiana na serikali kuondoa tofauti ya kijinsia kwenye dijitali, ili kuongeza ushiriki wa wanawake na wasichana katika teknolojia," alisema Lilian.

Mtaalamu wa Takwimu na Mwezeshaji wa Mafunzo ya Kidigitali kwa Watoto, Suna Salum, alitoa wito kwa mashirika ya ndani na kimataifa kuwezesha upatikanaji mafunzo na miundombinu.

"Mfano unaona WhatsApp imetoka wapi au inafanyaje kazi, ni kwamba nyuma ya mfumo huo iwapo na ifanye kazi kitendo hicho tunakiita 'coding', serikali pekee haiwezi kufanikisha tunachokitarajia.

"Ushirikiano kati ya serikali na mashirika binafsi utasaidia kupatikana vijana wengi ambao ni wabunifu tangu wakiwa na umri mdogo," alisema Suna.

Mfamasia Anna-Grace Malamsha alitoa wito kwa wasichana, kuzibaini na kuzitumia fursa zilizopo kwenye teknolojia ya kidigiti kwa kubuni miradi ili kukuza uchumi.

Alisema UN-Women imewawezesha kumudu kazi na kujikimu, kuwajengea ujasiri na kuhamasisha vijana wenzao kujikitika kwenye sayansi na teknolojia.

"UN Women imesaidia kubadili maisha yangu katika ujuzi kidigitali. Mimi pia ni mbunifu kurasa, kupitia mafunzo niliyoyapata nimefanya kazi na kampuni mbalimbali, nimepata kipato," alisema.



Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, David Silinde (kushoto), akisisitiza jambo kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian (kulia) na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, alipomtembelea ofisini kwake jijini Tanga kabla ya kuanza ziara ya siku moja wilayani Korogwe, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMAL ZUBERI**

## NHC yaita wawekezaji kwenye miradi yake

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limekaribisha wazawa na wageni kushirikiana kuwekeza kwenye miradi yake mbalimbali kwa ajili ya kupanua wigo wa kiuchumi na kuongeza ajira nchini.

Kaimu Meneja Mauzo na Masoko wa NHC, Emmanuel Lyimo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akishuhudia mwekezaji wa kwanza katika jengo la Morocco Square akifungua huduma ya hoteli.

Alisema NHC imeandaa mazingira mazuri ya uwekezaji, miongoni mwake mradi huo wa Morocco Square ulio na huduma mchanganyiko, ukiwa na majengo manne yakiwamo makazi, hoteli, ofisi na maduka.

"Mpaka sasa tumeshapata na tunajivunia kupata mwekezaji Kingjada Hotel kwenye jengo hili la NHC. Vilevile, hapahapa Morocco Square tumekwishauza asilimia 75 ya nyumba za makazi.

"Upande wa maduka tumeshapangisha kwa asilimia 100, ofisi pia tumeuza na kupangisha na zimebaki sehemu chache. NHC tunatoa wito kwa Watanzania na wawekezaji wote kutumia fursa hii, kuchangamkia sehemu zilizobaki," alisema.

Lyimo alisema NHC imefungua milango ya miradi ya uwekezaji ya ubia, akisema shirika hutoa eneo huku mwekezaji akijenga kama ambavyo sasa shirika hilo linaendelea kuboresha baadhi ya majengo yake ya Kariakoo, jijini.

Ofisa Rasilimali Watu wa Hoteli hiyo, Yohana Julius, alisema wametoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 100 kwenye idara tofauti kama vile upishi, mgahawa, usafiri, mapokezi, masoko na eneo la kufanyia mazoezi.

"Eneo linafikika kirahisi. Ninatoka wito kwa wawekezaji wengine kuona vyema kuwekeza katika miradi ya NHC ambayo miundombinu yake inamridhisha mwekezaji," alisema Yohana.

Mradi wa Morocco Square uliwekwa jiwe la Msingi na Rais Jakaya Kikwete mwaka 2015, ukigharimu Sh. bilioni 150.

Eneo la mradi lina ukubwa mita za mraba 110,000. Mradi una majengo manne, likiwamo la makazi na kiwanja cha ndege juu ya jengo.

# Waliojifungua wakiwa na umri mdogo wafunzwa ujasiriamali

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MABINTI 490 kati yao 386 waliojifungua watoto wakiwa na umri mdogo, wamenufaika na mafunzo mbalimbali yakiwamo ya ujasiriamali yaliyowawezesha kujiajiri na kuendesha maisha yao.

Inaelezwa kuwa mafunzo hayo yamewasaidia kutoingia kwenye hatari ya biashara haramu ya kujiuza kwa ajili ya kupata kipato.

Wasichana hao waliojifungua na kutelekezwa na wenzi wao wamepatiwa mafunzo hayo kupitia mradi wa kuboresha fursa za vijana wa Kitanzania kuweza kujiajiri na kuondokana na umasikini (SET) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswis kupitia Ubalozi wa Uswisi nchini.

Akizungumza na vijana hao, Mratibu wa Mawasiliano wa Shirika la Swiscontact, ambao ndio watekelezaji mradi huo, Masunga Isumbi, alisema vijana hao walionufaika ni kutoka kata za Berega, Chanzuru, Msowero, Mtumbatu, Mvumi, Rudewa na Ulaya wilayani Kilosa kupitia taasisi za MVIWAMORO,CSCA na CRESD ambazo zilipewa jukumu hilo na SET.

Vijana hao wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 wamenufaika kupitia mafunzo ya ujasiriamali ikiwamo ushonaji, uanzishaji biashara, uchakataji vyakula na usindikaji maziwa yaliyofanyika wilayani.

Alisema pamoja na vijana hao kuweza kujiajiri, baadhi yao wameokolewa pia katika hatari ya kujiingiza katika biashara haramu ya kuuza miili kutokana na kukosa kipato cha kuendesha maisha yao.

Alisema mradi wa SET umenufaisha jumla ya wanafunzi 559 (wavulana 69 na wasichana 490). Kati ya wasichana wanufaika, 386 ni waliojifungua wakiwa na umri mdogo.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana cha Upendo cha Kata ya Ulaya, wilayani Kilosa, Tausi Lyadiga, alisema kuwa kabla ya mafunzo hayo baadhi yao walikuwa wanategemea kujipatia kipato kwa kurubuniwa na wanaume kufanya mapenzi.

"Una mtoto mdogo, anahitaji kula na hela huna, mwanamume aliyekuzalisha ndio kama hivyo amekutelekeza, basi unajikuta unarubunika kwa wanaume wengine kujipatia kipato, anaweza kukupatia Sh. 2,000 mpaka 5,000," alisema Tausi.

Pili Simba, mkazi wa Kijiji cha Ulaya ambaye ni mnufaika wa mafunzo hayo, alisema yamemsaidia kuanzisha saluni ya kike ambayo kwa siku inamwingizia kati ya Sh. 15,000 na 50,000. Ameacha kuwa tegemezi kwa wazazi wake.

"Mimi nina mtoto, hivyo biashara ya saluni inanipa kipato kikubwa, ninaweza kujimudu kimaisha na pia ninafanya shughuli za kilimo cha mpunga na ufuta, navyo vinanilipa, ninapata fedha za kutosha," alisema Pili.

Mnufaika mwingine, Zuhena Yasini, alisema kuwa baada ya mafunzo hayo yalitolewa na SET juu ya ujasiriamali, pamoja na kushiriki katika kikundi chao, aliamua kujiongeza na kujifundisha ufundi cherehani na baadaye alinunua cherehani yake na kuanza kushona nguo huku akifanya biashara nyingine ya mgahawa. Sasa ana uhakika wa kupata fedha ya kuendesha maisha yake.

Pamoja na mkakati huo, kuzaa katika umri mdogo ni kosa kisheria. Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009, pia Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, zinaelekeza adhabu ya kifungo cha miaka 30 na wakati mwingine kifungo cha maisha kwa mtu anayethibitika kufanya mapenzi na mtoto.



# Teknolojia akili mnemba yaleta matokeo chanya sekta ya elimu

**Na Godfrey Mushi,**
ARUMERU

MATUMIZI ya teknolojia ya akili mnemba yameanza kuwa na mwitikio chanya katika utekelezaji wa sera mpya ya elimu nchini, huku baadhi ya wadau wa sekta hiyo wakiwamo walimu, wakieleza namna wanafunzi wanavyotumia mifumo ya Tehama katika kujibu maswali.

Akizungumzia mafanikio na changamoto za TEHAMA, wakati wa uzinduzi wa maabara ya kompyuta katika shule hiyo iliyopata ufadhili wa Kampuni ya Wilderness Technology Alliance ya Marekani, Mkuu wa Shule ya Sekondari Nkoasenga iliyoko Halmashauri ya Meru mkoani Arusha, alisema teknolojia hiyo ni nzuri, licha ya kuja na changamoto zingine.

Kampuni ya Wilderness Technology Alliance ya Marekani, imeanzisha mradi wa kuchagiza masomo ya TEHAMA, kwa shule za sekondari katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

"Ulimwengu wa leo unaenda kasi sana kidijitali. Tumefikia hatua ya kutumia akili mnemba. Hapa tuna kompyuta mpakato 20 tulizopewa na marafiki zetu kutoka Marekani, tumezipokea kwa mikono miwili na tunawashukuru sana," alisema.

Ofisa Elimu Sekondari, Halmashauri ya Meru, Marcel Itambo, alisema serikali ina mkakati wa kuanzisha mazungumzo na Kampuni ya Wilderness Technology Alliance ya Marekani, kwa ajili ya uimarishaji wa uijifunzaji na ufundishaji wa TEHAMA.

Kabla ya kukabidhi mradi huo kwa serikali, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Wilderness Technology Alliance ya Marekani, Lou August, alisema siku 15 za wataalam wa kampuni hiyo kutoka Marekani na Tanzania, wanaojitolea zimetosha kuacha mazingira sawa ya ufundishaji na ujifunzaji wa TEHAMA.

Timu hiyo ya wataalamu wa TEHAMA kutoka Marekani, inaongozwa na Lou August, Debora Grass, Dami Kehinde na Steve Popovich, wakati timu ya Tanzania inaundwa na Heke Hindo na Pendo Raphael.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Shirika la World Vision Tanzania (WVT), Easther Mshendwa, alisema World Vision, ni mdau wa masuala ya elimu, hasa masomo ya Tehama katika shule za sekondari, ndiyo maana wameona ni muhumi wakashiriki mradi huo, ili kuunga mkono serikali katika mabadiliko ya mitaala mipya iliyoanza kutumika mwaka huu.

Mratibu wa Mradi wa TEHAMA-Tanzania, anayeiwakilisha Kampuni ya Wilderness Technology Alliance ya Marekani, Upendo Raphael, alieleza kuwa kwa awamu ya kwanza, mradi huo unatekelezwa katika Mkoa wa Arusha (Arumeru), na Babati (Mkoa wa Manyara).



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa (kushoto), akimkabidhi cheti cha shukrani Meneja Manunuzi wa Barrick, Victor Ndamugoba, kutokana na kampuni hiyo kuwa mdhamini mkuu wa jukwaa la tatu la utekelezaji na ushirikishwaji Watanzania katika sekta ya madini uliomalizika mwishoni mwa wiki mkoani Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania waitwa kuwekeza viwanda vya bidhaa migodini

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amewaalika Watanzania na wawekezaji kuchangamkia fursa za uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa zinazotumika migodini.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akifunga Jukwaa la Tatu la Utekelezaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini lenye kauli mbiu ya "Uwekezaji wa Viwanda vya Uzalishaji wa Bidhaa za Migodini kwa Maendeleo Endelevu".

"Tuwashirikishe jukwaa lijalo ili waje wajifunze kitu na tutumie fursa hiyo kuibua fursa zingine ambazo sisi kama Tanzania, ambayo tumeshasema sisi ni kitovu cha madini na sasa madini haya tunayatafsiri katika kuyaongezea thamani na kuyaongezea thamani ni njia ya kuyajengea viwanda," alisema.

Aidha, alielekeza umuhimu na kuhakikisha viwanda wanavyosisitiza vijengwe, kwa ajili ya kutoa huduma kwenye migodi nchini.

Alisema: "Lakini siyo kujenga tu vinahitaji ujuzi. Ni muhimu sana tunaweza tukaanzisha hivi viwanda na kwa sababu vinahitaji taaluma ambayo hatuna, tukalazimika kutafuta wadau kutoka nje na wale wadau wanaweza wakaja Watanzania wakawa wanajifunza tu kwa vitendo, bila kupata ujuzi stahiki."

Hivyo, alitoa wito uanzishaji wa viwanda uende sambamba na ujengewaji uwezo Watanzania, kwa kuwapeleka shule, wapate ujuzi stahiki ili wamudu kuendesha viwanda hivyo.

Alisema baada ya kupata ujuzi baadaye watachukua nafasi za wataalamu waliopo nchini, ambao wanawaagiza kama wateja wao kutoka nje ya nchi.

Pia alishauri Watanzania kuona fursa za ndani kupitia vyuo kama vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) wanaweza kuhakikisha vijana wanaandaliwa kuchukua nafasi katika viwanda hivyo.

Dk.Kiruswa alishauri pia kuangalia jinsi ya kubadilishana wanafunzi na vyuo vya nje ili kujengeane uwezo.

Alisema anatumaini watakuwa na mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa suala la ushirikishwaji Watanzania kwa wamiliki wa leseni na watoa huduma katika sekta ya madini nchini.

Katibu Mtendaji Tume ya Madini, Yahya Samamba, alisema lengo la jukwaa hilo, kuhakikisha viwanda vinajengwa ndani ya nchi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na kusambaza kwenye migodi.

# Kinamama, watoto 300,000 wanufaika na kitita cha uzazi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KITITA cha Uzazi Salama (SBBC), kimewanufaisha kinamama na watoto 300,000 kwa awamu ya kwanza, huku awamu ya pili ikitarajiwa kuwanufaisha watu zaidi ya 600,000 katika mikoa mitano.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Haydom, inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Paschal Mdoe, alisema kitita hicho kilikuwa kinatoa huduma kwa vituo vya afya 30 katika mikoa mitano kwa awamu ya kwanza.

Alisema kwa awamu ya pili ambayo imeanza kutekelezwa, kitita hicho kitatekelezwa katika vituo 150 kwa mikoa hiyo.

Aliitaja mikoa ambayo imo kwenye kitita hicho na imepunguza vifo vya mama na watoto wachanga ni Shinyanga, Mwanza, Geita, Tabora na Manyara ambayo ilikuwa na idadi kubwa ya vifo isipokuwa Manyara.

Aidha, alisema idadi ya watoto waliokuwa wanafariki ndani ya siku moja wamepungua kwa asilimia 40, akisema kati ya watoto 10 waliokuwa wanafariki sasa hivi vinatokea vifo vinne mpaka vitano tu.

Kadhalika, alisema kutokana na kufanya vizuri ndiyo maana nchi ya Ethiopia, Kenya na Nigeria zimefika ili kujifunza namna ya kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Alisema nchi ya Sudani Kusini tayari imeshapewa mafunzo na Hospitali ya Haydom na nchi ya Rwanda, Botswana na Uganda wanaendelea kupewa maarifa.

Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Ahmad Makuwani, alisema kitita hicho kimekuwa mkombozi kwa mikoa hiyo ambapo ujauzito endapo unatishia mama ajifungue mtoto njiti anapewa dawa ya kumsaidia.

Alisema endapo mama akijifungua mtoto njiti anapewa msaada ili aweze kupumua vizuri.

Dk. Makuwani alieleza kuwa kitita pia kinamfuatilia mama akiwa kwenye nyakati za uchungu, mtoto aweze kulia mapema na mapigo ya moyo ya mtoto.

Alisema mwaka 2018 zilikuwapo hospitali 14 zilizokuwa na wodi maalum za kuwaangalia watoto wachanga wanaozaliwa na matatizo ila mpaka sasa zipo hospitali 241 nchini.

Alisema mpango wa serikali ni kila Hospitali ya Wilaya kuwa na wodi maalumu kwa ajili ya watoto njiti.

Mkurugenzi Msaidizi Afya ya Watoto na Vijana kutoka Wizara ya Afya, Dk. Felix Bundala, alikiri kuwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa mikoa mitano vimepungua.

Dk. Bundala alisema katika vifo 100 vilivyokuwa vinatokea vilisababishwa na upungufu wa ujuzi wa watoa huduma ambao umetibiwa na kitita cha uzazi salama.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema mkoa huo kwa awamu ya kwanza ya kitita walikuwa na vituo sita vilivyonufaika, sasa awamu ya pili vitakuwa vituo 30.

Dk. Kayera alisema kwa sasa vifo vimebaki 68 kati ya vizazi hai 100,000 kutoka vifo 100 katika vizazi hai 1000.

Mfadhili kutoka Global Financing Facility (GFF,) Dk. Alison Morgan, alisema kitita cha uzazi salama ni mfano wa kuigwa na nchi zingine, huku akiwashukru wahisani wenzake ambao wameshirikiana kuleta matokeo chanya ya upatikanaji wa huduma na kuokoa maisha ya watoto na wajawazito.





# Milioni 34/- zamaliza kero upatikanaji maji Urambo

**Na Mwandishi Wetu,** URAMBO

WAKAZI zaidi ya 6,000 wa Kitongoji cha Kitega Uchumi Wilaya ya Urambo mkoani Tabora, wameondokana na tatizo la ukosefu wa maji baada ya Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One kuwajengea kisima.

Kisima hicho kilichogharimu Sh. milioni 34, kitahudumia kaya 671 za kitongoji hicho ambazo awali zililazimika kufuata huduma ya maji umbali mrefu.

Akizindua kisima hicho, Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Elibariki Bajuta, aliipongeza kampuni hiyo na kuiomba kuendelea kuisaidia zaidi katika sekta ya uchumi.

Kadhalika, aliwaonya viongozi wa kitongoji hicho kutowatoza fedha kinamama wanaochota maji, akisema kampuni iliyochimba kisima imetoa huduma hiyo bure kwa wakazi wa eneo hilo.

"Nikipata taarifa zozote za malalamiko kutoka kimamama hawa kuwa wamelipishwa hela za maji nitaanza na Mwenyekiti wa Kitongoji, nitakupumzisha sehemu salama wakati nashughulikia tatizo lako, nafikiri mnanifahamu huwa siongea jambo mara mbili," alisema.

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya Alliance one, David Mayunga, alisema kampuni hiyo ina utaratibu wa kuchangia huduma za jamii katika maeneo inayonunua tumbaku hasa katika sekta za afya, mazingira na elimu na kwamba kisima hicho ni sehemu ya utekelezaji wa utaratibu wao.

"Kabla ya kuchimba kisima hiki tulifanya utafiti na kubaini tatizo la maji katika Kitongoji cha Kitega Uchumi ndipo tukaamua kuchimba kisima chenye urefu wa mita 150 kwenda chini, kujenga mnara wa tangi la maji pamoja na usambazaji, kazi zilizogharimu kiasi hicho," alisema Mayunga.

Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Urambo, Petro Kisasi, alisema upatikanaji wa maji Urambo ni asilimia 24.5 na uzalishaji unategemea visima virefu saba ambavyo uwezo wake ni kuzalisha maji mita za ujazo 388 kwa siku, wakati mahitaji ni lita milioni 3.6 kwa siku.

Baadhi ya wananchi wa kitongoji hicho akiwamo, Rosemarry Yusuph, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwaondolea kero ya maji katika eneo hilo.

Asia Athumani alisema walikuwa wakienda kuchota maji ya kunywa katika kijiji cha jirani cha Kilimahewa ambako walikuwa wananunua ndoo moja kwa Sh.50.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kitega Uchumi, Fredrick Alloyce, alisema awali wananchi wake walikuwa watumia maji ya visima vifupi ambavyo sio salama kwa matumizi ya kunywa.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa Wilaya ya Urambo alizitaka kampuni za ununuzi wa tumbaku kuhakikisha zinawalipa wakulima ndani ya wiki mbili baada ya kuchukua mazao yao.

Alisema hatasita kukamata magari na kufunga milango yote ya ofisi ya kampuni itakayoshindwa kufanya hivyo wilayani kwake.

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya Alliance One (AOTL), David Mayunga, alitoa rai kwa wakulima wa tumbaku, kuboresha kilimo ili kupata madaraja mazuri.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (katikati), akisaidiana na wakulima wa pamba wilayani Kishapu juzi, kuweka pamba kwenye mizani kwa ajili ya kuipima ili kuiuza, huku akiwataka wakulima wote wa pamba mkoani humo kulima kilimo chenye tija ili wapate mavuno mengi na kuinuka kiuchumi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakulima wa pamba walia na bei elekezi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAKULIMA wa pamba wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wamelalamikia bei elekezi ya serikali inayowataka kuuza zao hilo kwa Sh.1,150 kwa kilo, wakisema siyo rafiki kwao na inazidi kuwaletea umaskini.

Walieleza kero hiyo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha alipotembelea baadhi ya vituo vya kununua zao hiyo.

Mmoja wa wakulima hao, James Ally, alisema bei elekezi haimtoi mkulima kwenye umaskini bali inaendelea kumkandamiza na ndiyo sababu wananchi wengi wameachana na kilimo hicho.

"Ukilima hekari moja kuanzia maandalizi ya shamba hadi kuvuna tunatumia zaidi ya Sh.260,000, na katika hekari hiyo zinatoka kilo 200, sasa ukiuza kilo kwa Sh.1,150 unapata Sh.230,000 hapo tayari una hasara ya Sh.30,000 na bado kuna gharama zingine tumeziacha," alisema Ally.

Naye Nicodemas Masesa, alisema zao hilo halipewi hadhi yake kama mazao mengine ikiwamo tumbaku ambalo kila msimu bei yake inapanda lakini tofauti na pamba ambayo inashuka.

Akizungumza baada ya kupokea kero hizo, Macha, alisema bei ya pamba huwa inatoka kwenye soko la dunia, hivyo hawawezi kuipinga.

Aliwataka wakulima kwamba ili wapate kunufaika na kilimo hicho wanapaswa kufanya kilimo chenye tija kwa kulima kisasa na kupata mavuno mengi.

Alisema endapo mkulima atalima kisasa atapata mavuno hadi 2,000 kwa hekari moja na kutoka kwenye kilo 200 ambayo haiwezi kuwatoa kwenye umaskini.

**Walieleza kero hiyo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha alipotembelea baadhi ya vituo vya kununua zao hiyo.**

# Wataka kurejea utamaduni 'shikome' kudhibiti ukatili

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake na watoto katika Kata ya Mwamala Manispaa ya Shinyanga wameitaka jamii ya Wasukuma kurejesha utamaduni wa kufanya vikao vya jioni vya kimaadili katika koo zao (shikome), ili kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti na kueleza kuwa kukosekana kwa vikao hivyo kumesababisha wanawake na watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na kukosa sehemu ya kusema.

Walisema vikao hivyo vilikuwa vinawapatia nafasi ya kueleza changamoto zinazowakabili na kuelimishana masuala mbalimbali ya maisha.

Mkazi wa Kijiji cha Bunonga, Ester Mandi akizungumza na Nipashe kufuatia utekelezaji wa mradi wa nafasi ya wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), alisema kukosekana kwa vikao kumechangia kwa asilimia kubwa ongezeko la ukatili huo.

Alisema baadhi ya wazee wanakaa kwenye vijiwe vya kahawa, mabanda ya televisheni na baa mpaka saa sita usiku, hawana muda wa kukaa na familia na kuzungumza nao kama ilivyokuwa miaka ya zamani.

Mkazi wa Kijiji cha Ibanza, Anna Nkinga alisema, shikome iliwasaidia wanawake kupaza sauti zao pindi wanapoonewa, hivyo kukosekana kumesababisha ongezeko la matukio ya ukatili, huku kukiwa hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kutokana na wao kukosa msaada.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kayange, alisema, utandawazi umechangia kupoteza baadhi ya mila na tamaduni za kabila hilo ambazo awali zilikuwa na faida na zilichangia kulinda maadili na kukemea wale wanaopotoka.

Akitoa takwimu za ukatili dhidi ya watoto na wanawake kwa mwaka 2019/22, Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Shinyanga, Aisha Omari, alisema mpaka kufikia Desemba mwaka 2023 wanafunzi 59 walipewa ujauzito, ubakaji 56 na ulawiti wa matukio tisa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA JERRY W. SILAA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25



MHE. JERRY WILLIAM SILAA
**WAZIRI**



MHE. GEOPHREY MIZENGO PINDA
**NAIBU WAZIRI**



ENG. ANTHONY D SANGA
**KATIBU MKUU**



LUCY D. KABYEMERA
**NAIBU KATIBU MKUU**





# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA JERRY W. SILAA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**); Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2023/24. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa **15** wa Bunge la **12** ambao ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu aliyonikabidhi kwa juhudi, uadilifu na weledi ili kuleta ufanisi na kukuza ustawi na maendeleo ya wananchi kupitia sekta ya ardhi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka ya kuongoza Taifa letu. Katika kipindi hiki cha uongozi wake, Sekta ya Ardhi imepata mafanikio mbalimbali ambayo yanajumuisha uboreshaji wa sera, sheria, taratibu na mifumo ya utoaji wa huduma; kuongezeka kwa kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini; uendelezaji wa makazi; kurahisishwa kwa taratibu za upatikanaji wa haki za ardhi; utatuzi wa migogoro ya ardhi; na utoaji wa elimu kwa umma.

4. ***Mheshimiwa Spika***, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru kwa maelekezo na ushauri wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia maslahi na ustawi wa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kudumisha Muungano wetu ambao umetimiza miaka **60**.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nakupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza na kusimamia kwa umahiri shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi shughuli za Bunge kama Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima ili muweze kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za Bunge kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imewasilisha utekelezaji wa malengo ya Serikali kwa mwaka 2023/24, pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2024/25.

   Kwa hakika, hotuba hiyo imetoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi katika kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na uhakiki na upimaji wa mipaka ya vijiji kama njia mojawapo ya kudhibiti migogoro ya ardhi. Ninaahidi kuwa, Wizara itayafanyia kazi masuala yote yaliyoainishwa katika hotuba hiyo ili kufikia malengo ya Serikali yaliyokusudiwa.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) kwa utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi. Maoni na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara umesaidia kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi. Tunawaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri wao ili kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa sekta ya ardhi inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi, kuimarisha usalama wa milki na kudhibiti migogoro ya ardhi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani na pongezi za dhati ...................
   kwa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa maelekezo, miongozo, ushauri na ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Ukonga kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa kwa kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, kipekee kabisa, naishukuru familia yangu kwa kuwa karibu nami na kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu.
   Kadhalika, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zinanipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu.

**Salamu za Pole**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kumuenzi kwa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kisiasa nchini.
11. ***Mheshimiwa* Spika**, mwezi Februari, 2024, Taifa letu lilipata msiba wa kuondokewa na aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo mahiri. Kipekee, natoa pole kwa Mheshimiwa Fredrick Edward Lowassa kwa kuondokewa na Baba yake mpendwa. Aidha, natoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, familia na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Kwahani, Zanzibar na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Mbarali. Hakika michango yao itaendelea kukumbukwa.

12. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali kutokana na maafa, ajali na majanga yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini.

    Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka watanzania wenzetu waliojeruhiwa ili waweze kupona na kurejea katika shughuli zao za kila siku za ujenzi wa Taifa. Aidha, tunamwomba Mwenyezi Mungu awalaze marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/25. Bajeti ya Wizara imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26); Mpango Mkakati wa Wizara; Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano ya Kikanda na Kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Maeneo ya kipaumbele yatakayotiliwa mkazo na Wizara katika mwaka 2024/25 ni pamoja na:-
    (i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi mijini na vijijini;
    (ii) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;
    (iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;
    (iv) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na
    (v) Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24 NA MALENGO YA MWAKA 2024/25.**

**Mapato na Matumizi**

14. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **163.17** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni **43.43** ziliidhinishwa kwa ajili ya Mishahara (PE); Shilingi Bilioni **37.61** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi Bilioni **82.13** kwa ajili ya miradi ya maendeleo (DEV). Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, Shilingi Bilioni **14.01** ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni **68.12** ni fedha za nje. Aidha, kutokana na mahitaji, Wizara iliongezewa bajeti ya Shilingi Bilioni **287.66** kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni, Watumishi na Wakandarasi. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia Shilingi Bilioni **450.83**.

15. ***Mheshimiwa Spika***, hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya Shilingi Bilioni **423.13** zilipokelewa, sawa na asilimia **93.86** ya bajeti ya Shilingi Bilioni **450.83.** Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **34.72** ni mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi sawa na asilimia **79.94** ya bajeti husika; Shilingi Bilioni **21.94** ni matumizi mengineyo ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia **56.24** ya bajeti husika na Shilingi Bilioni **366.47** ni miradi ya maendeleo sawa na asilimia **99.48**. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa, Shilingi Bilioni **309.53** ni fedha za ndani sawa na asilimia **99.52**; na Shilingi Bilioni **56.94** ni fedha za nje sawa na asilimia **99.26**.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Fungu **48** ilipanga kukusanya shilingi bilioni **300**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imekusanya shilingi bilioni **136** sawa na asilimia **45.3** ya lengo**.**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jukumu la ukusanyaji wa maduhuli kuhamishiwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara imeendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha kupendekeza jukumu la kukusanya kodi ya pango la ardhi liendelee kutekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na iwezeshwe kwa kurudishiwa sehemu ya fedha (*retention*) kwa ajili ya makusanyo. Pendekezo hili linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo: ukusanyaji wa kodi ya pango la Ardhi ni jukumu la kisheria lililoainishwa chini ya kifungu cha 25 na 33 cha Sheria ya Ardhi (Sura 113); ukusanyaji unahitaji wataalamu wa sekta ya ardhi ambao Wizara ndio mamlaka yao ya ajira na nidhamu; na mfumo wa TEHAMA wa Wizara unaotunza kumbukumbu za wamiliki umeunganishwa na shughuli kuu za kisekta za upangaji, upimaji, uthamini na umilikishaji ardhi na hivyo kupunguza changamoto za ukusanyaji zilizokuwepo hapo awali.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni **250** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Lengo hili litafikiwa kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli kidigitali; kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na usajili wa ardhi; kuendelea kufuatilia madeni ya kodi ya pango la ardhi kutoka katika mashirika, taasisi za umma na wamiliki binafsi; na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

**Mapato na Matumizi ya Fungu Na. 03**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (**Fungu 03**) iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **8.2.** Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **2.49** ni mishahara ya watumishi (PE); shilingi bilioni **2.29** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC); na shilingi bilioni **3.41** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2024, Tume imepokea jumla ya Shilingi Bilioni **7.33** kati ya bajeti ya Shilingi Bilioni **8.82** sawa na asilimia **83.11** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi Bilioni **1.37** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); Shilingi Bilioni **2.55** ni Mishahara; na Shilingi Bilioni **3.41** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Tume ilipanga kukusanya shilingi milioni **18** kutokana na kodi ya pango la nyumba zilizopo Tabora. Hadi, tarehe 15 Mei, 2024 shilingi milioni **9.5** zimekusanywa sawa na asilimia **53** ya lengo. Aidha, Tume ilipanga kuhamasisha wadau kuchangia kiasi cha shilingi milioni **700** kwa ajili ya shughuli za upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya shilingi bilioni **2.77** zilipokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali.

**UANDAAJI WA HATIMILIKI NA USAJILI WA NYARAKA**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuandaa Hatimiliki **500,000,** Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000.** Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000** na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**. Hadi tarehe **15 Mei, 2024**, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki **87,240** sawa na asilimia **17.4** ya lengo na Hati za Hakimiliki za Kimila **21,953** sawa na asilimia **4.2** ya lengo. Kwa upande wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, jumla ya vyeti **56** vimeandaliwa sawa na asilimia **56** ya lengo, Hati za Sehemu ya Jengo **324** sawa na asilimia **32.4** ya lengo na miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **95,456** sawa na asilimia **95.4** ya lengo zimesajiliwa.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza kasi ya umilikishaji, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi; Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma; na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi na kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji zilizokiuka maadili. Aidha, Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ilichukua hatua ya kupunguza gharama za umilikishaji kwa zaidi ya asilimia 50. Hatua hiyo imeongeza kasi ya umilikishaji wa ardhi ambapo Hatimiliki zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka Hatimiliki **76,746** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Mei, 2023 mpaka Hatimiliki **87,240** kwa kipindi cha Julai, 2023 mpaka Mei, 2024. Vilevile, utoaji wa Hatimiliki umeongezeka kutoka Hatimiliki **67,331** mwaka 2020/21 hadi Hatimiliki **86,398** mwaka 2022/23 kutokana na huduma za ardhi kuanza kutolewa katika Ofisi za Ardhi za Mikoa.

    **Nawahimiza wananchi kote nchini kuendelea kutumia Ofisi za Ardhi za Mikoa kupata huduma na fursa ya punguzo la tozo za**



umilikishaji kuhakikisha kuwa wanamilikishwa maeneo yao kwa mujibu wa sheria.

24. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kuandaa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000**, Hatimiliki **500,000,** Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **1,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**. Vilevile, miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za kisheria **100,000** zitasajiliwa.

**Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji**

25. *Mheshimiwa Spika,* Wizara inaratibu na kusimamia ardhi ya uwekezaji kwa kushirikiana na taasisi za uwekezaji nchini ili kuhakikisha ardhi kama rasilimali muhimu inaleta tija kiuchumi na kijamii. Usimamizi huu unahusisha ugawaji na usimamizi wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kupitia Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, maombi **191** ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta **11,613.08** yaliidhinishwa kwa ajili ya uwekezaji ambapo kati ya hayo maombi **61** ni ya raia wa Tanzania na **130** ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Uwekezaji wa nje una mtaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni **704.21** sawa na shilingi Trilioni **1.82**.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kupitia Kliniki za Ardhi**

26. *Mheshimiwa Spika,* kliniki za Ardhi ni mpango wa Wizara wenye lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wote wenye kuhitaji huduma au wenye changamoto za ardhi wanapatiwa huduma karibu na maeneo wanayoishi kwa haraka na ufanisi unaotarajiwa na jamii. Kwa kutambua hilo, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imekuwa ikiendesha zoezi la kliniki za ardhi kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo wataalam wa kada zote za ardhi wanakuwepo eneo moja kwa wakati mmoja hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma zote za ardhi papo kwa papo. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Mei, 2024 kliniki za ardhi zimefanyika katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Viongozi wa Wizara, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Kwa kutambua umuhimu wa kliniki za ardhi na matokeo chanya yanayopatikana, Viongozi Wakuu wa Wizara wamefanya ziara kwenye majiji yote nchini na kushirikana na viongozi wa maeneo hayo kushughulikia changamoto za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi. Majiji hayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma na Tanga. **Napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kote nchini ambao wameshirikiana kwa karibu sana na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa na wataalamu wa sekta ya ardhi katika kuendesha na kusimamia Kliniki za ardhi katika maeneo yao**.

27. *Mheshimiwa Spika*, kliniki za ardhi zimeonesha mafanikio kutokana na wananchi wengi kujitokeza kusikilizwa kwa uhuru na uwazi kisha changamoto zao kupatiwa ufumbuzi kwa haraka. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, wananchi **35,963** walihudumiwa katika mikoa **22** iliyoendesha kliniki za ardhi. Migogoro na malalamiko **7,444** yaliyopokelewa ambapo migogoro na malalamiko **4,565** yalishughulikiwa. Aidha, Hatimilki **17,553** zilikamilishwa na kukabidhiwa kwa wamiliki na maombi mapya ya hati **13,289** yalipokelewa. Katika kliniki hizo, jumla ya shilingi bilioni **3.03** zilikusanywa kama tozo na ada mbalimbali za kisheria.

28. *Mheshimiwa Spika,* kufuatia uendeshaji wa zoezi la Kliniki za Ardhi, Wizara imebaini vyanzo mbalimbali vya malalamiko na migogoro ya ardhi. Vyanzo hivyo ni pamoja na madai ya fidia, utolewaji wa milki pandikizi, uvamizi wa maeneo ya umma na binafsi, udanganyifu na utapeli kwa kutumia nyaraka za kughushi, ucheleweshaji wa huduma, mwingiliano wa mipaka, madai ya mali za urithi au wanandoa, utekelezaji wa miradi ya urasimishaji na upimaji shirikishi na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi kuhusu masuala ya umiliki wa ardhi.

29. *Mheshimiwa Spika,* Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kuchukua hatua kwa wananchi wanaotumia nyaraka za kughushi au kuvamia viwanja vyenye umiliki kwa kuwafikisha mahakamani na kurejesha maeneo hayo kwa wamiliki halali. Aidha, Wizara imeanzisha Dawati Maalum katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ili kuwezesha wananchi wenye migogoro ya ardhi hasa yenye sura ya jinai kuwasilisha malalamiko yao ili yapatiwe ufumbuzi. **Natoa wito kwa wananchi na wadau wote wa ardhi wenye changamoto zinazotokana na vitendo vya dhuluma kuendelea kujitokeza kutoa malalamiko yao ili kuiwezesha Wizara kuchukua hatua stahiki.**

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji 975**

30. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaratibu utekelezaji wa Maelekezo ya Baraza la Mawaziri kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ya vijiji na Mitaa **975** nchini. Katika utekelezaji wa maamuzi haya, tathmini imebainisha kuwa vijiji na mitaa yenye migogoro ni **1,004** (Vijiji 981 na Mitaa 23) badala ya **975** kama ilivyobainishwa hapo awali.

31. *Mheshimiwa Spika*, hadi tarehe 15 Mei, 2024 utekelezaji wa uamuzi katika vijiji **438** na mitaa **13** umekamilika na utekelezaji katika vijiji **543** na mitaa **10** unaendelea**.** Utekelezaji huo umewezesha ardhi yenye ukubwa wa ekari milioni **2.4** kumegwa na kurejeshwa kwa wananchi ikijumuisha ekari milioni **1.65** kutoka kwenye maeneo ya hifadhi, ranchi na mashamba ya Serikali; ekari **707,962** kutoka kwenye Mapori Tengefu **12** na ekari **46,715** kutoka kwenye Hifadhi za Misitu saba (**7**).

Vilevile, maeneo **18** kati ya **20** yamefanyiwa uthamini na kiasi cha shilingi bilioni **178.57** kinahitajika kwa ajili ya kuhamisha wananchi kutoka kwenye maeneo ya Hifadhi na vyanzo vya maji. Kati ya maeneo yaliyothaminiwa, wananchi wa maeneo sita (**6**) wamelipwa fidia kiasi cha shilingi bilioni **20.1.**

32. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha usimamizi wa mipaka ya Hifadhi, vigingi **32,838** vimesimikwa na mkuza kuchongwa kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa **21**, Mapori ya Akiba **29** na Hifadhi za Misitu **416**. Pia, Serikali kupitia Tangazo la Serikali Na. 754 la tarehe 20/10/2023, imerekebisha mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa kumega eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba **478** kwenda kwa wananchi. Utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri utakamilishwa kwa kumalizia kazi za uthamini na kulipa fidia; upimaji upya wa vijiji vinavyomegewa maeneo; kushughulikia maeneo yenye changamoto zaidi ambayo yanahusisha baadhi ya vijiji vitakavyoondolewa katika maeneo ya hifadhi, vyanzo vya maji na maeneo muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama wa Nchi. Utekelezaji wa kazi hizo umepangwa kukamilika ifikapo Juni, 2024. Mwelekeo wa Wizara ni kuweka mifumo thabiti ya usimamizi na ufuatiliaji kwa kushirikiana na wadau wote muhimu ili kupunguza migogoro mikubwa kama hii kuendelea kujitokeza.

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

33. *Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kuhakikisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanaundwa na kufanya kazi katika Wilaya zote nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 jumla ya Mabaraza **139** yameundwa ambapo kati ya hayo Mabaraza **104** yanatoa huduma. ***Napenda kutumia fursa hii kuzihimiza Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Wilaya kuwezesha upatikanaji wa majengo ya ofisi na Wajumbe wa Baraza ili Mabaraza 35 yaliyobaki yaweze kutoa huduma.***

34. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kushughulikia mashauri **33,250**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 Wizara imeshughulikia mashauri **29,573** ambapo mashauri mapya ni **14,093** na mashauri ya zamani ni **15,480**. Kati ya hayo, mashauri **15,550** yameshughulikiwa na kutolewa uamuzi na mashauri **14,023** yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kusimamia Mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ili kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2024/25 Wizara itashughulikia mashauri **14,023** yaliyobaki na mengine yatakayojitokeza.

**UTHAMINI WA MALI**

35. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu na kusimamia uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini **54,000** ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za fidia zenye wafidiwa **34,000** na kushughulikia malalamiko **30** ya uthamini wa fidia. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **57,285** sawa na asilimia **111.66** ya lengo ambapo kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **22,311** na taarifa za uthamini wa fidia **34,974.** Aidha, malalamiko **91** ya fidia yalipokelewa na kushughulikiwa. Vilevile, Wizara imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kufanya uthamini wa mali za wananchi wa Ngorongoro wanaohama kwa hiari kupisha shughuli za uhifadhi. Uthamini umefanyika kwa awamu sita **(6)** katika kata **11** na vijiji **25** ambapo mali za kaya **650** zenye thamani ya shilingi bilioni **3.79** zimefanyiwa uthamini.

36. *Mheshimiwa Spika*, kumekuwepo malalamiko yanayohusu ulipaji wa fidia kutoka katika maeneo mbalimbali nchini. Malalamiko hayo yanatokana na wananchi kutofahamu kwa hakika wadau wanaohusika na ulipaji wa fidia; baadhi ya taasisi kufanya uthamini wa fidia bila kuwepo fedha kwa ajili ya malipo ya fidia; na kutozingatiwa kwa taratibu za uhakiki wa taarifa za uthamini wa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, Sura 138.

Ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, Wizara imetoa Waraka wa Uthamini na Fidia Na. 1 wa Mwaka 2024 ambao pamoja na mambo mengine unaelekeza taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa shughuli za uthamini, uhakiki wa taarifa za uthamini na ulipaji wa fidia. **Naomba ifahamike kuwa, jukumu la Wizara ni kuratibu uthamini na wajibu wa kulipa fidia ni wa taasisi itakayonufaika na uthamini huo. Aidha, natoa wito kwa wadau wote wa uthamini kuhakikisha wanazingatia Waraka wa Uthamini na Fidia.**

37. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2024/25, Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini **54,000.** Kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na taarifa za uthamini wa fidia **34,000**.

**UPANGAJI NA UENDELEZAJI WA MIJI NA MAKAZI**

38. *Mheshimiwa Spika,* upangaji miji na makazi ni mojawapo ya majukumu ya msingi ya Wizara ambayo yanaratibiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na taratibu za uendelezaji miji. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira na kuwa na uhakika wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji.

**Udhibiti na Usimamizi wa Uendelezaji Miji (*mabadiliko ya matumizi ya ardhi*).**

39. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kumekuwepo na ongezeko la ukuaji wa miji na kusababisha hitaji kubwa la kubadili matumizi ya ardhi, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za Viwango vya Kupanga Ukubwa wa Ardhi kwa matumizi mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Pia, imeboresha Kanuni ya Makundi ya Matumizi na Madaraja ya Matumizi ili kuwezesha matumizi ya ardhi kushabihiana hivyo kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi. Vilevile, katika Kanuni hiyo mchakato wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi umeboreshwa ambapo maombi yatajadiliwa katika ngazi ya mtaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ndipo yajadiliwe na Kamati za Halmashauri ili kuimarisha ushirikishwaji wa wadau hivyo kupunguza migogoro ya ardhi.

40. *Mheshimiwa Spika*, maeneo ya wazi yanapaswa kusimamiwa, kutunzwa na kulindwa ili yatumike kwa maslahi mapana ya umma. Hata hivyo, maeneo hayo yamekuwa yakivamiwa na kubadilishwa matumizi au kutumiwa vinginevyo kutokana na sababu nyingi zikiwemo uvamizi wa makusudi, kutolipwa fidia kwa wamiliki wa asili, kutumika kama vyanzo vya mapato ya Halmashauri na usimamizi usioridhisha wa Mamlaka zilizopewa kusimamia maeneo hayo. Ili kukabiliana na matumizi holela ya maeneo hayo, matumizi ya maeneo ya wazi yamewekewa utaratibu wa kuidhinishwa na Wizara endapo yatahitajika kutumika kwa maslahi ya nchi. **Napenda kusisitiza kuwa maeneo ya wazi ni lazima yatunzwe, yalindwe na kudumishwa ili yatumike kwa manufaa ya umma yakiwemo kufanyia mikutano ya hadhara, kupendezesha mandhari na mazingira ya mji, michezo kwa watoto katika mitaa, watu kupumzika, kufanyia chanjo kwa umma na kutumika kama hifadhi ya watu na misaada wakati wa maafa, majanga au dharura.**

41. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu na kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi **500**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, maombi **465** sawa na asilimia **93.2** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliidhinishwa. Katika mwaka 2024/25 Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi **500** kwa kuzingatia sheria na kanuni za mipangomiji.

**Urasimishaji wa Makazi**

42. *Mheshimiwa Spika,* Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 zinaelekeza kuwa maeneo ya makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa yatarasimishwa. Katika kutekeleza matakwa ya sera hizi, Wizara imeendelea kuratibu urasimishaji wa makazi yaliyoendelezwa bila kupangwa kwa kuishirikisha jamii, asasi za kiraia na sekta binafsi. Katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kurasimisha makazi **300,000**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya makazi **237,424** sawa na asilimia **79.1** yamerasimishwa katika Mamlaka za Upangaji **37**.

43. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2024/25, Wizara itarasimisha makazi **500,000**. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na Sekta Binafsi inaendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi ambao bado makazi yao hayajarasimishwa ili kukamilisha zoezi hilo na kuendeleza kliniki za ardhi ili kukwamua urasimishaji katika maeneo ambayo hayajakamilisha miradi ya urasimishaji. Ili kufikia lengo la kurasimisha makazi **500,000** katika mwaka 2024/25, Wizara itaanza na kukwamua urasimishaji ambao ulikwama kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uchangiaji hafifu wa wananchi na baadhi ya kampuni zilizofanya urasimishaji kutokamilisha kazi kwa wakati. Mathalan, katika mkoa wa Dar es Salaam urasimishaji haukukamilika katika mitaa **270**. Ili kukwamua kazi hizo, Wizara itaajiri wataalam wa muda wa mipangomiji na upimaji na kuhakikisha kazi hizo zinakamilika. Zoezi hili limeanza kutekelezwa katika mitaa **13** ya mkoa wa Dar es Salaam. ***Natoa Wito kwa wananchi ambao makazi yao hayajarasimishwa kujitokeza kurasimishiwa.***

**USIMAMIZI WA MILKI KUU**

44. *Mheshimiwa Spika,* pamoja na majukumu mengine, Wizara ina jukumu la kusimamia Milki Kuu nchini. Sekta ya Milki inajumuisha ardhi iliyopangwa na kupimwa kwa kujengwa nyumba za makazi, majengo ya biashara, viwanda, maeneo ya burudani na majengo ya matumizi maalum. Wadau wa Sekta ya Milki wanajumuisha wawekezaji, wamiliki wa majengo, wapangaji, taasisi za fedha, mawakala, wanunuzi wa nyumba na viwanja na watafiti wa soko la nyumba. Sekta hii imeendelea kukua na kuvutia wadau wengi zaidi kutokana na fursa za uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo soko la fedha na nyumba za kupangisha.

45. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha usimamizi wa sekta hii, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kukamilisha uandaaji wa Sheria na kanuni za kusimamia Sekta ya Milki Kuu, kutoa elimu kwa wadau na kuandaa kanzidata ya Waendelezaji Milki pamoja na mawakala wa Milki. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mapendekezo ya Kutunga Sheria ya Milki yameandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka ya uamuzi.

Mapendekezo hayo pamoja na mambo mengine yanalenga kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Milki '*Real Estate Regulatory Authority*' ili kuongeza tija na ufanisi katika usimamizi na uratibu wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa nchi.

**UPIMAJI NA RAMANI**

**Upimaji wa viwanja na mashamba**

46. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuratibu, kusimamia na kuidhinisha viwanja **500,000** na mashamba **500**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, viwanja **249,340** na mashamba **7,559** yamepimwa na kuidhinishwa sawa na asilimia **49.87** ya lengo la viwanja na asilimia **1,511.8** ya lengo la mashamba. Ongezeko kubwa la mashamba yaliyopimwa na kuidhinishwa linatokana na mpango wa Serikali wa kuhamisha wananchi kutoka katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera na Saunyi mkoani Tanga. Katika mwaka 2024/25, Wizara itasimamia upimaji na uidhinishwaji wa viwanja **500,000** na mashamba **500**.

**Utayarishaji wa Ramani**

47. *Mheshimiwa Spika,* ramani ni zao la kazi za upimaji ardhi, ambalo huweza kupatikana katika mfumo wa nakala ngumu au nakala tete. Ramani huzalishwa kutokana na taarifa za msingi za kijiografia. Ramani zinazotayarishwa zinajumuisha za viwanja, mashamba, mipaka ya kiutawala na kimataifa na Hifadhi za Taifa. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, ramani za mipaka ya kiutawala ya Wilaya **17** katika Mikoa ya Dar es Salaam (**5**), Kagera (**7**), Dodoma (**2**), Tanga (**1**), Arusha (**1**) na Mbeya (**1**) zimeandaliwa. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuandaa ramani za mipaka ya kiutawala ya Wilaya **25**. Mwelekeo wa Wizara ni kuwa na Ramani za kidigitali ili kurahisisha upatikanaji wa ramani.

48. *Mheshimiwa Spika,* kumekuwepo na changamoto ya uandaaji wa ra-

mani unaofanywa na baadhi ya taasisi na sekta binafsi bila kuzingatia sheria na ubora hali inayosababisha kuwepo kwa tafsiri zisizo sahihi za mipaka ya kimataifa na kiutawala.

Matokeo yake ni kuwepo kwa migogoro ambayo ingeweza kuzuilika endapo taratibu za uandaaji wa ramani zingezingatiwa kwa mujibu wa Sheria ya Upimaji, Sura 324. **Naelekeza taasisi zote za umma na binafsi zizingatie takwa la kisheria linalompa mamlaka Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kuandaa na kuidhinisha ramani zote zikiwemo za mipaka ya kiutawala na kimataifa**.

**Upimaji wa Mipaka ya Vijiji**

49. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kuratibu na kupima mipaka ya vijiji ambapo katika mwaka 2023/24, ilipanga kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **100.** Hadi tarehe 15 Mei, 2024, jumla ya vijiji **742** imehakikiwa na kupimwa mipaka. Kati ya hivyo, vijiji **475** vimehakikiwa na kupimwa upya mipaka yake na upimaji wa vijiji **267** ambavyo vilikuwa havijapimwa umefanyika. Aidha, migogoro ya mipaka ya vijiji vitano (**5**) vya Bangalala, Mwembe, Makanya, Mgwasi na Nasuro katika Wilaya ya Same imetatuliwa. Vilevile, mgogoro wa mipaka kati ya shamba la Malonje (Efatha) na vijiji vitano (**5**) vya Sikaungu, Msandamuungano "A", Msandamuungano "B", Songambele Azimio na Malonje katika Wilaya ya Sumbawanga umetatuliwa. Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji **1,000**. ***Natoa rai kwa mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa Vijiji vinavyoanzishwa vinapimwa mipaka yake kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.***

**Upangaji na Upimaji wa Viwanja Mbadala vya Waathirika wa Maporomoko ya Mlima Hanang'**

50. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyotokana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Kufuatia maafa yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang' kutokana na kuporomoka kwa sehemu ya Mlima Hanang', Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga na kupima viwanja mbadala vya waathirika wa maporomoko hayo. Viwanja hivi vimepimwa kutoka katika eneo la ekari 100 zilizomegwa kutoka shamba la Jeshi la Magereza lililopo katika kijiji cha Gidagamowd, Wilaya ya Hanang'.

Jumla ya viwanja **269** vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo makazi (235), makazi na biashara (15), biashara (7) na huduma za jamii (12). Aidha, waathirika wote **108** wamepatiwa viwanja kwa ajili ya makazi.

**Upangaji na Upimaji wa Viwanja na Mashamba kwa ajili ya Wananchi Wanaohama kwa Hiari Kutoka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

51. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii (Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro) inaendelea na upimaji wa viwanja na mashamba kwa ajili ya makazi, kilimo na ufugaji. Kazi hii inafanyika katika vijiji vya Msomera (Handeni) na Saunyi (Kilindi) katika Mkoa wa Tanga ambapo lengo ni kupima viwanja **10,000** na mashamba **8,500.** Hadi tarehe 15 Mei, 2024, viwanja **5,031** vya makazi vyenye wastani wa ukubwa wa ekari **2.5** na mashamba **7,897** yenye ukubwa wa wastani wa ekari **5** yamepimwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji ikiwemo mvua kubwa zilizonyesha, Wizara imejipanga kukamilisha upimaji wa mashamba ifikapo Juni, 2024.

**HUDUMA ZA TEHAMA**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango wa Wizara ni kuifanya TEHAMA kuwa nyenzo muhimu ya kuendesha shughuli za sekta ya ardhi. Lengo la hatua hiyo ni kuongeza uwazi, ufanisi, uwajibikaji, kupunguza gharama na muda wa utoaji huduma. Wizara imekamilisha usanikishaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi kwa kutumia watalaam wa ndani. Hatua inayoendelea ni kuhamisha taarifa kutoka kwenye mifumo ya zamani na majalada kwa awamu kwenda kwenye Mfumo ulioboreshwa. Aidha, mfumo utaanza kutumika kwa awamu ya kwanza katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Mbeya, Mwanza na Dodoma ifikapo Juni, 2024.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kusimika na kusambaza miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa **25** na Halmashauri **132**.

Hadi tarehe 15 Mei, 2024, usimikaji wa miundombinu wezeshi ya TEHAMA katika Halmashauri **44** umekamilika na kazi ya usimikaji wa miundombinu hiyo inaendelea katika Halmashauri **41**. Pamoja na huduma nyingine, miundombinu hii itatumika katika utoaji wa huduma za ardhi kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Huduma za Ardhi.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilizikopesha Mamlaka za Serikali za Mitaa **57**, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa, Chuo Kikuu Ardhi na Vyuo vya Ardhi vya Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA) shilingi bilioni **50** kwa ajili ya kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Wizara imeendelea kufuatilia marejesho ya fedha hizo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Shilingi billioni **23.7** zimerejeshwa na Halmashauri **55** ambapo Halmashauri **13** zimerejesha mikopo yao kwa asilimia **100**; Halmashauri **42** zimerejesha sehemu ya fedha; na Halmashauri mbili (**2**) za Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Musoma hazijarejesha kabisa. Napenda kuzipongeza Halmashauri za Jiji la Mwanza; Manispaa za Morogoro, Ilemela na Kigamboni; Miji ya Tunduma na Bariadi; Halmashauri za Wilaya za Moshi, Meru, Kilosa, Geita, Kaliua, Songwe na Mbozi zilizotekeleza wajibu wa kurejesha fedha kwa mujibu wa makubaliano. ***Naungana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuzitaka Halmashauri na Taasisi ambazo hazijarejesha au hazijakamilisha marejesho, kurejesha fedha wanazodaiwa ifikapo Juni, 2024 ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kunufaika na fedha hizo. Kwa halmashauri ambazo hazitatekeleza agizo hilo, fedha hizo zitakatwa moja kwa moja kutoka kwenye ruzuku zao.***

55. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuepuka changamoto zilizojitokeza kwenye utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa awamu ya kwanza, Wizara imefanya maboresho katika utaratibu huo. Maboresho yaliyofanyika yanahusisha fedha kutolewa kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa; fedha kutolewa kwa awamu kwa kuzingatia hatua ya kazi iliyofikiwa; na fedha za mauzo ya viwanja kuwekwa kwenye akaunti maalum ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara imebuni na kusanifu Mradi wa *Msalato Satellite City* katika Jiji la Dodoma utakaokidhi mahitaji ya watu zaidi ya **14,776**. Mradi huo utawezesha ujenzi wa makazi bora yenye miundombinu na huduma muhimu za jamii na biashara za aina mbalimbali hivyo kupunguza msongamano wa wananchi wanaofuata mahitaji katikati ya mji. Katika mwaka 2024/25, Wizara imepanga kubuni na kusanifu miji ya Satelaiti miwili (2) katika majiji ya Dodoma (Msalato) na Arusha (Afcon City) ili kuwa na miji nadhifu na kudhibiti makazi holela. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za mfuko ili kuwezesha halmashauri kupanga na kupima miradi iliyoandaliwa. Vilevile, Wizara kupitia Programu ya KKK itapanga, kupima na kumilikisha viwanja **100,000** kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi.

**Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi**

57. ***Mheshimiwa Spika;*** mwaka 1991/92, Serikali ilianzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja (Plot Development Revolving Fund – PDRF) ambao ulilenga kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji viwanja. Hata hivyo, mwaka 2016 Serikali ilisitisha matumizi ya akaunti za mifuko mbalimbali nchini ikiwemo akaunti ya Mfuko huu. Kusitishwa kwa matumizi ya akaunti kuliikosesha Wizara chanzo cha uhakika cha fedha za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia umuhimu wa upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini, Serikali imeridhia kurejeshwa kwa matumizi ya akaunti ya Mfuko wa Maendeleo ya Ardhi.

Kwa kuanzia, Serikali imetoa mtaji wenye thamani ya shilingi bilioni **15.4** na imeridhia marejesho ya fedha kiasi cha shilingi bilioni **50** za Kupanga, Kupima na Kumilikisha zinazodaiwa kwenye mikopo ya Halmashauri ziingizwe kwenye Mfuko huu. Ili kuwezesha uendelevu wa mfuko na ufanisi katika utekelezaji, Mwongozo wa Uratibu na Usimamizi wa Mfuko umeandaliwa. Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kurejesha matumizi ya akaunti ya mfuko.

**Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP). Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Mradi huu ilipanga kupima mipaka ya vijiji **700**; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji **700**; kuandaa na kuidhinisha Hati za Hakimiliki za Kimila **200,000;** na kukarabati ofisi za ardhi za Halmashauri **41**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, mipaka ya vijiji **407** imepimwa, vyeti vya ardhi ya kijiji **320** vimetolewa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **843** imeandaliwa katika Halmashauri **21**. Aidha, vipande vya ardhi **381,509** vimetambuliwa kwa ajili ya kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila katika Wilaya sita (**6**) za Tanganyika (**69,216**), Maswa (85,182), Mbinga (56,547), Mufindi (72,991), Songwe (77,514) na Chamwino (20,059).

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, jumla ya makazi **500,000** yalipangwa kurasimishwa katika Halmashauri **23**, kuanza kusimika vituo **22** vya upimaji na kuweka alama za msingi za upimaji **276**. Hadi tarehe 15 Mei 2024, vipande vya ardhi **62,200** vimerasimishwa katika Halmashauri za Jiji la Dodoma (**7,545**), Wilaya ya Chalinze (**12,112*)***, Manispaa ya Kigoma (**6,171**), Mji wa Nzega (**11,796**), Manispaa ya Kahama (**10,860**) na Manispaa ya Shinyanga (**13,716**); na Alama za Msingi za Upimaji **327** zimewekwa katika Halmashauri **26** sawa na asilimia **118** ya lengo.

Aidha, zabuni kwa ajili ya urasimishaji makazi **400,000** imetangazwa. Vilevile, Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji **22** amepatikana na kazi ya ujenzi itaanza katika mwaka 2024/25.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa majengo **25** ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kujenga kumbi za mihadhara nne (**4**) katika vyuo vya ardhi vya Tabora na Morogoro. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Washauri Elekezi wa ujenzi wa majengo **25** ya Ofisi za Ardhi za Mikoa na kumbi nne (**4**) za mihadhara za Vyuo vya Tabora na Morogoro wamepatikana na wameanza kazi za awali za ubunifu katika maeneo ambayo ujenzi utafanyika. Vilevile, Mradi umeboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuwezesha ununuzi wa samani za ofisi, vitendeakazi na magari **18.**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2024/25 kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) ni kuhakiki na kupima mipaka ya vijiji na kutoa vyeti vya vijiji **1,000**; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **1,000**; kuandaa Mipangokina ya vijiji **100** na kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila **300,000**; kurasimisha vipande vya ardhi **100,000** kupitia wataalam wa Serikali na vipande **400,000** kupitia kampuni zinazofanya kazi za urasimishaji; kubadilisha Nyaraka za ardhi (Data conversion) **1,921,758** kutoka analojia kwenda kidijitali; kuwezesha upatikanaji wa miundombinu kwa ajili ya usambazaji wa mfumo wa ILMIS kwa Ofisi za Ardhi **67**; kusanifu na kusimika Vituo vya Kieletroniki vya Upimaji (CORs) **22**; na kujenga mfumo wa kidigitali wa Vitalu vya Thamani ya Ardhi nchini. Kazi nyingine zinatakozotekelezwa kupitia Mradi ni kujenga Ofisi za Ardhi za Mikoa **25**; kujenga kumbi za mihadhara katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora - ARITA (**2**) na Morogoro - ARIMO (**2**); kuwezesha ubunifu na ujenzi wa Jengo la Taifa la Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi; kukarabati Ofisi za ardhi katika Halmashauri **34**; kukamilisha taratibu za ununuzi wa magari **52**; kununua vifaa, kuhuisha mitaala na kuwezesha ukuzaji wa ujuzi wa watumishi wa Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro; kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya **30**; na kuandaa na kuboresha sera, sheria na miongozo mbalimbali.

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

63. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kujenga na kuongeza alama, kuzipima, kukarabati zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa mikataba ya mipaka. Katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuimarisha sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **80** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **100**. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara iliendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya kwenye kipande cha kilomita **110** kutoka Namanga hadi Tarakea ambapo kazi hiyo imekamilika. Katika mwaka 2024/25, Wizara itakamilisha uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **100** kutoka Tarakea mpaka Ziwa Jipe na sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi yenye urefu wa kilomita **100.**

**TAASISI NA BODI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Nyumba la Taifa lina jukumu la kujenga nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha; kujenga majengo kulingana na mipango iliyoidhinishwa na Serikali; kuzalisha na kuwezesha uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kusimamia milki za majengo; kufanya ukarabati; kukusanya kodi ya pango; kutoa huduma ya ushauri elekezi, upangaji wa maeneo na ukandarasi wa majengo. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia Mpango Mkakati wa Shirika wa miaka 10 (2015/16 – 2025/26).

***Ujenzi wa nyumba za makazi na majengo mengine kwa ajili ya kuuza na kupangisha***

**(i) Mradi wa Kawe 711, Golden Premier Residence na Morocco Square**

65. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2023/2024 Shirika lilipanga kukwamua miradi mikubwa iliyopo Kawe iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 ikiwemo mradi wa nyumba **422** wa Kawe 711 wenye thamani ya Shilingi Bilioni **169** na Mradi wa *Golden Premier Residence* wa nyumba **196** ambao una thamani ya shilingi bilioni **71**. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Mradi wa Kawe 711 unaendelea na umefikia asilimia **35** na unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2026. Aidha, mradi wa *Golden Premier Residence* (GPR) bado umesimama na majadiliano kati ya Shirika na mkandarasi yanaendelea.

66. ***Mheshimiwa Spika;*** Shirika limeendelea na uuzaji na upangishaji wa majengo katika Mradi wa *Morocco Square* ambapo katika jengo lenye nyumba za makazi **100**, nyumba **71** zimeshauzwa na mauzo ya nyumba zilizobaki yanaendelea. Aidha, upangishaji wa Hoteli yenye vyumba **81** umefanyika kwa asilimia **100**, maduka (Retail Mall) asilimia **94** na ofisi asilimia **42**.

**(ii) Mradi wa *Samia Housing Scheme***

67. ***Mheshimiwa Spika;*** shirika limeanza utekelezaji wa Mradi wa Samia Housing Scheme wenye nyumba **5,000**. Katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **560** Kawe Jijini Dar es Salaam na nyumba **500** katika Jiji la Dodoma maeneo ya Ndejengwa, Iyumbu na Medeli. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, ujenzi wa nyumba **560** awamu ya kwanza katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia **60** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Ujenzi wa Majengo ya Biashara***

68. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika Mikoa ya Kagera (Bukoba), Mwanza, Dodoma, Shinyanga (Kahama), Morogoro, Mtwara (Masasi) na Lindi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024 ujenzi wa majengo ya maduka **50** katika Mji wa Kahama umefikia asilimia **14** na ujenzi wa jengo la biashara katika mji wa Masasi umeanza.

***Utekelezaji wa Sera ya Ubia ya Shirika***

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shirika lilipanga kutekeleza miradi **24** ya ubia yenye thamani ya Shilingi Bilioni **340** kupitia Sera yake ya Ubia ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2024, Shirika limeidhinisha na kusaini mikataba ya miradi **21** yenye thamani ya Shilingi Bilioni **271**. Miradi hii itatekelezwa kwa muda wa miezi **24** ambapo utekelezaji umeanza Januari, 2024 katika Mikoa ya Dar es Salaam (**17**), Mwanza (**3**) na Iringa (**1**).

70. ***Mheshimiwa spika,*** kupitia miradi hii, Shirika linatarajia kupata manufaa mbalimbali ikiwemo kuongeza idadi ya nafasi za upangaji, mathalan, katika eneo la Kariakoo nafasi za upangishaji zitaongezeka kutoka **324** hadi **2,691**. Hivyo, mapato, thamani ya mali za Shirika na faida ya uwekezaji kwa kuzingatia eneo (Return on Investments) itaongezeka.

***Ukarabati wa Nyumba za Shirika***

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha ukarabati wa majengo **181** ambayo yana nyumba **3,111** katika mikoa **15** ya Shirika. Aidha, jumla ya majengo **83** ambayo yana nyumba **451** yaliyopo katika mikoa mbalimbali ya Shirika yanaendelea kufanyiwa ukarabati.

***Ukusanyaji wa Mapato ya Shirika***

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Shirika lilipanga kukusanya Shilingi Bilioni **274** kutokana na vyanzo mbalimbali ambavyo ni kodi

ya pango Shilingi Bilioni **105**, ukandarasi Shilingi Bilioni **99** na Shilingi Bilioni **70** kutokana na mauzo ya nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Shirika limekusanya jumla ya Shilingi Bilioni 208.5 sawa na asilimia **76.1** ya lengo.

Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **90.4** ni makusanyo ya kodi ya pango, makusanyo ya kodi ya mauzo ya nyumba na viwanja ni Shilingi Bilioni **50.8** na Shilingi Bilioni **60.9** ni mapato yanayotokana na miradi ya ukandarasi.

***Ukusanyaji wa Madeni ya Shirika***

***73. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, shirika limekusanya Shilingi Bilioni **7.2** ambapo shilingi Bilioni **4.1** ni deni la pango la nyumba, Shilingi Bilioni **2.7** kutoka kwenye miradi ya ukandarasi na Shilingi Milioni **400** ni madeni mengineyo ikiwemo ya uuzaji wa nyumba. Madeni hayo yamepungua kutoka Shilingi Bilioni **25.7** Julai, 2023 hadi Shilingi Bilioni **18.5** Aprili, 2024 sawa na asilimia **28**. Hata hivyo, shirika bado linakabiliwa na changamoto ya wadaiwa sugu wa kodi ya pango; wapangaji kutokulipa kwa wakati; wakandarasi na wanunuzi wa nyumba kutokukamilisha malipo yao kwa wakati. Hivyo, shirika limeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo. **Natoa wito kwa wapangaji kulipa ankara zao kwa wakati na wadaiwa wote kulipa madeni yao mapema kabla hatua zaidi hazijachukuliwa kwa ukiukaji wa mikataba.**

***Ujenzi wa Miradi ya Ukandarasi***

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shirika limeendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara nane (**8**) yenye thamani ya shilingi bilioni **194** katika Mji wa Serikali Mtumba ambao umefikia wastani wa asilimia **81**; ujenzi wa jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wenye thamani ya shilingi bilioni **9.8** ambao umefikia asilimia **75**; na ujenzi wa majengo manne (**4**) ya Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA) katika mikoa ya Simiyu, Songwe, Dodoma na Pwani yenye thamani ya shilingi bilioni **2.8** ambao umekamilika kwa asilimia **100**. Vilevile, ujenzi wa Kituo cha Biashara ya Madini ya Tanzanite wenye thamani ya shilingi bilioni **5.5** katika mji wa Mirerani Mkoa wa Manyara ambao umefikia asilimia **85**; na ujenzi wa jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) wenye thamani ya shilingi bilioni **3.1** Jijini Dar Es Salaam ambao umefika asilimia **99**.

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, shirika limepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuendelea na ujenzi wa nyumba **422** katika mradi wa Kawe 711 ambao unatarajiwa kufikia asilimia **75** ifikapo Juni, 2025; kuendelea na ujenzi wa nyumba **196** katika mradi wa *Golden Premium Residence (GPR)*; kuanza ujenzi wa nyumba **560** za Mradi wa *Samia Housing Scheme* (SHS) awamu ya pili katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam; kuendelea na ujenzi wa nyumba **150** za *Samia Housing Scheme* katika eneo la Medeli na Iyumbu Jijini Dodoma kwa ajili ya kuuzia wananchi; na kukamilisha ujenzi wa majengo ya biashara katika mkoa wa Shinyanga (Kahama) na kuendelea na ujenzi katika mji wa Masasi (Mtwara).

***76. Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zitakazotekelezwa na Shirika ni kuanza ujenzi wa majengo ya biashara katika miji ya Moshi, Arusha, Tanga, Tabora, Lindi, Morogoro, Bukoba na Dar es Salaam; kuendelea na ujenzi na usimamizi wa miradi **21** ya ubia yenye thamani ya Shilingi billioni **271**; kuendelea kutekeleza mpango wa matengenezo kwa kukarabati majengo **250**; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo kukamilisha ujenzi wa jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kituo cha Biashara ya Madini ya Tanzanite Mirerani; kuendelea kutekeleza shughuli za utaalam elekezi/ushauri katika miradi mbalimbali nchini; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) Jijini Dodoma na Zanzibar.

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

***77. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia shughuli za Upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Utekelezaji wa majukumu ya Tume unazingatia Mpango Mkakati wa Tume (2021/22-2025/26).

***Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji***

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume ilipanga kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano **(5)** na Vijiji **210** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Mipango hii huandaliwa kwa njia shirikishi na kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara kupitia Tume imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **339** katika wilaya **27** sawa na asilimia **161.4** ya lengo la mwaka. Ongezeko la vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi linatokana na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji Usalama wa Milki za Ardhi na mwitikio wa wadau wa ndani na nje ya nchi kuchangia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Uandaaji wa Mipango hii umefanya kuwa na jumla ya Vijiji **4,126** vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kati ya vijiji **12,318** vilivyopo nchini.

***79. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Tume itaendelea kuratibu uandaaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi inayotekelezwa kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP) na kuwezesha kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **422** kwa kushirikiana na Mamlaka za upangaji na wadau wa kimkakati katika maeneo mbalimbali ya miradi ya kimkakati, migogoro, mpakani na yenye uzalishaji mkubwa wa mazao. Aidha, Tume itaendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano (**5**). ***Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini kutoa kipaumbele katika kutenga fedha za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili kuongeza kasi ya uaandaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.***

**Bodi za Wataalam wa Fani za Ardhi**

***80. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia Bodi za Wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji; Bodi ya Usajili wa Wathamini; na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi yanajumuisha kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi na maadili ya kitaaluma.

**Vyuo vya Ardhi vya Morogoro na Tabora**

***81. Mheshimiwa Spika***, Vyuo vya Ardhi Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA) vimeendelea kutekeleza majukumu ikiwemo kufanya utafiti na kutoa mafunzo ya muda mrefu katika ya fani mbalimbali za sekta ya ardhi. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia vyuo hivyo iliahidi kudahili wanafunzi **2,000** (ARITA **1,500** na ARIMO **500**). Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa jumla ya wanafunzi **1,744** walidahiliwa ambapo Chuo cha Ardhi Tabora kilidahili wanafunzi **1,256** na Chuo cha Ardhi Morogoro kilidahili wanafunzi **488** katika mafunzo ya Astashahada na Stashahada. Aidha, wanafunzi **1,602** wamehitimu mafunzo yao. Vilevile, Wizara iliahidi kukamilisha ujenzi wa Maktaba ya Chuo cha Ardhi Tabora ifikapo Juni, 2024. Fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maktaba hiyo zimetolewa na kazi inaendelea.

***82. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara kupitia vyuo vyake inatarajia kudahili wanafunzi **2,670** (ARITA **1,580** na ARIMO **1,090**). Aidha, kutokana na ongezeko la mahitaji ya wataalam wa sekta ya ardhi, Chuo cha Ardhi Morogoro kitaongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi **489** hadi **1,090**. Vilevile, Wizara itakamilisha ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

**UTAWALA NA RASILIMALI WATU**

***83. Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara ina jumla ya watumishi **2,395** kati ya hao wanaume ni **1,679** na wanawake ni **716**.

Aidha, katika kipindi hicho Wizara ilipata kibali cha kuajiri Watumishi **98** wa fani za Upimaji wa Ardhi, Uthamini na Utawala wa Ardhi. Aidha, watumishi **347** wamepandishwa vyeo na watumishi **37** wamebadilishwa kada. Watumishi **1,166** watapandishwa vyeo katika mwaka 2024/2025.

***84. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia nidhamu na uadilifu katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi nchini. Katika kusimamia nidhamu za watumishi, hatua mbalimbali kwa watumishi waliotuhumiwa kwa makosa mbalimbali zilichukuliwa ambapo watumishi **22** wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tuhuma za ukosefu wa maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma; Watumishi saba (**7**) waliachishwa kazi na watumishi wawili (**2**) walipewa onyo na kuwekwa chini ya uangalizi.

**Kuwajengea Uwezo Watumishi**

***85. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwawezesha kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwaongezea utaalam, ujuzi na maadili ili kuhakikisha wanakuwa na weledi zaidi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuwawezesha watumishi **215** kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **191.** Katika mwaka 2024/25, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi kushiriki mafunzo kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

**HABARI NA ELIMU KWA UMMA**

***86. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara iliahidi kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2024, Wizara imetoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi kupitia vipeperushi, majarida, mitandao ya kijamii, makala za magazeti, kliniki za ardhi, mikutano ya hadhara na vipindi vya redio na luninga.

Aidha, Wizara ilifanya mkutano mmoja (**1**) na wahariri wa vyombo vya habari pamoja na mikutano **11** ya waandishi wa habari kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi. Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia tovuti ya Wizara (www.lands.go.tz) na maonesho mbalimbali. Pia, elimu kwa umma imeendelea kutolewa kupitia kipindi cha Televisheni cha '*Maisha ni Nyumba'* kinachoratibiwa na Shirika la Nyumba la Taifa.

**SHUKRANI**

***87. Mheshimiwa Spika,*** kipekee nawashukuru Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb), Naibu Waziri; Mhandisi Anthony Damian Sanga, Katibu Mkuu; na Bi. Lucy Dominico Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu; kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya kusimamia sekta hii muhimu. Aidha, nawashukuru Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi; Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa; Prof. Wakuru Magigi Maseka, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Bi. Evelyne Mugasha, Mthamini Mkuu wa Serikali; na Bi. Stella Tullo, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Pia, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi; na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kutekeleza majukumu yao kwa bidii na maarifa na hivyo kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Wizara.

***88. Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, Shelter Afrique, African Union Boarder Program, Regional Centre for Mapping of Resources Development (RCMRD), Benki ya Maendeleo Afrika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC), Watumishi Housing Company Limited, taasisi za fedha za ndani, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi.

***89. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani kwa vyombo vya habari kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya sekta ya ardhi. Kwa hakika wanahabari wameiwezesha Wizara kuwafikia wadau wengi zaidi kwa namna mbalimbali.

***90. Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu Bi Mariam Bakari Silaa na mwanangu Simba William Silaa kwa uvumilivu na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu**.**

**HITIMISHO**

***91. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara katika mwaka 2024/25, itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa kuboresha huduma zinazotolewa. Ili kutekeleza azma hiyo, Wizara itazingatia vipaumbele vilivyoainishwa awali ambavyo ni:-

(i) Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi mjini na vijijini;
(ii) Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;
(iii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kum bukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;
(iv) Kuhakikisha uwepo wa nyumba bora, ukuaji wa sekta ya milki na maendeleo ya makazi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na
(v) Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/25**

***92. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kama ifuatavyo: -

***Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi***

| Na. | Maelezo | Aina | Makisio ya Bajeti ya mwaka 2024/25 |
|---|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | | 250,000,000,000 |
| | **Makisio ya Matumizi** | | |
| B | Matumizi ya Kawaida | Mishahara (PE) 48,435,318,000 | 48,435,318,000 |
| | | Taasisi (PE) | 1,720,210,000 |
| | | **Jumla ya Mishahara** | **50,155,528,000** |
| | | Matumizi Mengineyo (OC) | 35,399,978,250 |
| | | Taasisi (OC) | 1,243,068,750 |
| | **Jumla ya Matumizi Mengineyo (OC)** | | **36,643,047,000** |
| | **Jumla ya matumizi ya Kawaida** | | **86,798,575,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo | Ndani | 10,601,757,000 |
| | | Nje | 60,054,753,000 |
| | **Jumla ya Miradi ya Maendeleo** | | **70,656,510,000** |
| | **Jumla Kuu** | | **157,455,085,000** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Fungu **48** ni shilingi **157,455,085,000.00**.

***Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.***

| AINA | AINA YA MATUMIZI | SHILINGI |
|---|---|---|
| **A** | **Mapato** | |
| | **Mapato ya Serikali** | **18,000,000** |
| **B** | Matumizi ya Kawaida; | |
| | Mishahara | 3,887,780,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 3,244,318,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **7,132,098,000** |
| **C** | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Fedha za ndani | 5,041,232,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **5,041,232,000** |
| **JUMLA KUU (B+C)** | | **12,173,330,000** |

Jumla ya matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya **Fungu 03** ni Shilingi **12,173,330,000**.

***93. Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni Shilingi **171,372,508,000.00**.

***94. Mheshimiwa Spika***, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba imeambatana na majedwali yanayoainisha kwa ufasaha takwimu zinazohusiana na shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Aidha, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz.***

***95. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.



# Maandalizi kupiga 'stop' matumizi zebaki yaanza

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

SERIKALI imeanza maandalizi ya kuzuia matumizi ya zebaki kwenye uchenjuaji wa dhahabu kwa wachimbaji wadogo nchini, ili kuwaepusha na madhara yatokanayo na kemikali hiyo ikiwamo magonjwa ya mfumo wa fahamu.

Maofisa wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), pamoja na watafiti wa miamba (GST), wameanza kutoa elimu ya kuepuka madhara ya kemikali hiyo kwa wachimbaji.

Akizungumza na wachimbaji wadogo wa eneo la Matimba lililopo Kata ya Saza wilayani Songwe, Mhandisi wa Mazingira kutoka NEMC, Boniphace Kyaruzi, alisema kwa sasa wanawafundisha wachimbaji hao namna ya kuepuka madhara yatokanayo na kemikali hiyo.

Alisema mbali na kuwafundisha namna ya kuepuka madhara pia wanawafundisha mbinu mbadala ya kuchenjua dhahabu, ili waanze kujiandaa kuacha kutumia zebaki ambayo imebainika kuwa na madhara kwa binadamu na kwenye mazingira.

"Tunaipenda dhahabu lakini pia tunayapenda na maisha yenu, ninyi mmezoea kutumia zebaki kwa hiyo serikali haiwezi kusitisha matumizi ya kemikali hii ghafla, ndio maana imeanzisha mradi huu wa kuwafundisha kuepuka madhara wakati ikitafuta mbadala wa kudumu," alisema Kyaruzi.

Alisema wakati utakapofika wa kuzuia matumizi ya kemikali hiyo utaanzishwa utaratibu wa kuwachukulia hatua kali wale wote watakaokuwa wanakutwa wakitumia ama kuiuza.

Vilevile alisema watakuwa wanafunga migodi itakayokuwa inakuwa ikitumia kemikali hiyo kwenye uchenjuaji wa dhahabu, huku akidai kuwa mpaka sasa imeanza kuuzwa kwa kificho.

Mkemia Mwandamizi wa GCLA, Zabibu Duru alisema kemikali hiyo inaingia kwenye mwili wa binadamu kupitia kwenye macho, pua, mdomoni na kwenye ngozi na hivyo kuanza kusababisha madhara kwenye viungo vya ndani.

Alisema kemikali hiyo ikiingia kwenye mwili wa binadamu inaanza kuathiri viungo kama figo, ini na moyo hali ambayo inasababisha vifo kwa wachimbaji.

Zabibu alisema ili kujikinga na madhara ya kemikali hiyo wachimbaji wanatakiwa kuitumia wakiwa wamefunika maeneo muhimu ya miili ikiwamo kuvaa viatu vya mvua, kofia ngumu, mipira ya mikononi ili kukinga kemikali hiyo isigusane na ngozi.

Alisema kemikali hiyo inaanza kumuathiri binadamu taratibu na kadri miaka inavyozidi kwenda ndipo madhara huanza kuonekana zaidi na kwamba isipogundulika mapema inasababisha vifo.

Baadhi ya wachimbaji wadogo wa eneo la Matimba walisema wameitumia kemikali hiyo kwa muda mrefu na hawajawahi kupatiwa elimu na madhara yake hali ambayo ilikuwa inawafanya wasichukue tahadhari.

Mmoja wa wachimbaji hao, Vincent Siwale alisema kutokana na elimu waliyoipata walianza kubaini kwamba wameshapata madhara ya kemikali hiyo ila bado haijaanza kuleta madhara makubwa.

Alisema kuna wakati alikuwa anaugua bila kujua kinachomsumbua lakini alipokwenda hospitalini aliambiwa aache kutumia zebaki kwenye shughuli za uchimbaji kwa maelezo kuwa ndiyo iliyokuwa inamwathiri.

Katibu wa Chama cha Wachimbaji wilayani Songwe, Elius Pangani, aliwashukuru maofisa hao kwa kutoa elimu hiyo kwa wachimbaji wadogo kwa maelezo kuwa itawasaidia kupunguza madhara ambayo yamekuwa yakitokea.



Baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Matimba, Kata ya Saza wilayani Songwe, wakichenjua dhahabu kwa kutumia kemikali ya zebaki bila kuvaa vifaa vya kujikinga mwishoni mwa wiki. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

## H'shauri yaagiza wasimamizi barabara za mradi kutimuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imezitaka kampuni ya ujenzi ya Cico inayojenga jengo la maabara na barabara za mradi wa TACTIC na kampuni ya mhandisi ambayo ni mkandarasi mshauri kwenye miradi hiyo, kuwaondoa wasimamizi wake kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya halmashauri hiyo kutoridhishwa na kasi ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo unaogharimu Sh. bilioni 21 ambao ulianza Novemba 2023.

Akizungumza baada ya ziara ya kukagua ujenzi wa barabara za Kalobe-Itende, Machinjioni- Mapelele, Kabwe-Sido na Iziwa, Meya wa Jiji hilo, DorMohamed Issa alisema hawana uhakika kama mkandarasi atamaliza miradi hiyo kwa wakati uliopangwa kwa mujibu wa mkataba.

Alisema tangu mkandarasi huyo alipokabidhiwa mradi na kuanza kazi hakuna alichokifanya kwenye barabara zote, hali ambayo inasababisha wananchi kuendelea kukabiliwa na changamoto ya barabara licha ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Hivyo, alimtaka mkandarasi huyo kumwondoa Meneja Mradi, Penfeng Wang na mkandarasi mshauri, Jofrey Kanjanja kwa kushindwa kusimamia utekelezaji wa mradi sawa na makubaliano ya mkataba wao.

"Mkandarasi mshauri urafiki wako na mkandarasi unatupa wasiwasi, kazi haiendi na nyie kila wakati mko pamoja, hapo kazi haiwezi kwenda kwa sababu utashindwa kusimamia vyema mradi huu, nataka kampuni zenu zitubadilishie wasimamizi ili miradi yetu itekelezwe kwa wakati," alisema.

Katika hatua nyingine Meya huyo alimtaka mhandisi wa Jiji hilo, Leonard Mohosea kuhakikisha kila Jumatatu anawasilisha taarifa za mwenendo wa mradi na kumsimamia ipavyo mkandarasi, ili kufikia malengo ya mradi ambayo serikali imejiwekea.

# Wapatiwa mafunzo kudhibiti tembo kwenye makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ASKARI wa Jeshi la Uhifadhi Tanzania, wameanza kupatiwa mafunzo maalumu ya kuwadhibiti tembo wanaoingia kwenye makazi ya wananchi bila kusababisha madhara kwa wanyama hao.

Mafunzo hayo yanatolewa na Shirika la Mzinga lenye makao makuu yake mkoani Morogoro kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI).

Askari wanaopatiwa mafunzo hayo ni wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na Askari wa Vijiji (VGS).

Askari hao wanafundishwa namna ya kufukuza tembo kwa kutumia mabomu baridi ambayo yanatumika kuwafukuza wanyama hao bila kuwajeruhi na yalianza kutolewa wilayani Mbarali kwa maofisa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Pori la Akiba la Mpanga-Kipengele.

Akielezea bomu hilo la kufukuzia wanyama hao, Meja Erick Siara ambaye anatoka katika Shirika la Mzinga alisema mabomu hayo yatasaidia kupunguza migogoro ya wanyamapori na binadamu ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Alisema bomu hilo ni muunganiko wa vitu vitatu ambavyo ni pilipili, sauti ya mlipuko ambayo ni kubwa na mwanga ambavyo vyote kwa pamoja vinatumika kuwakimbiza wanyama.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Timotheo Mnzava aliwataka TAWIRI kuendelea kufanya utafiti ili kubuni njia nyingine mbadala za kukabiliana na tembo hao katika maeneo yote yanayopakana na hifadhi nchini.

Alisema wanyama hao wamekuwa wakizoea mbinu zinazotumika kuwafukuza na hivyo akasisitiza kuwa kuna uwezekano ikafika muda wakayazoea mabomu hayo na kuendelea kuwasumbua wananchi kwenye maeneo yao.

Mtafiti kutoka TAWIRI, Revocatus Mneney alisema kuwa utaratibu wa kufukuza tembo ni shirikishi na kwamba taasisi za Wizara ya Maliasili na Utalii zitaendelea kushirikiana na wananchi ili kuleta ufanisi wa mbinu zinazobuniwa.

Alisema mbali na mafunzo hayo lakini pia wananchi watakiwa kuendelea kutumia mbinu ambazo wamefundishwa na wataalamu mbalimbali katika maeneo yao.

Alisema kila mbinu inayobuniwa inatakiwa kuwa shirikishi na kwamba baadhi zinafundishwa hata kwa wananchi wa kawaida hasa ambao wanaishi kwenye maeneo ya pembezoni mwa hifadhi.

Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Hera Haima alisema mabomu baridi hayo yana kishindo kikubwa na mwanga mkali ambao wana uhakika utawakimbiza wanyama hao na kurudi hifadhini.

Alisema wana uhakika kuwa maeneo yote ambayo wanyama hao wamekuwa wakisababisha madhara kwa wananchi yatakuwa na usalama kutokana na mbinu hiyo kuwa na ufanisi.

# Kampeni kudhibiti usugu wa vimelea magonjwa yazinduliwa

**Na Gwamaka Alipipi**

OFISI ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), wamezindua kampeni iitwayo 'Holela-Holela Itakukost'.

Lengo la kampeni hiyo ni kushughulikia tatizo la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Uvida) na magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu (Zuonotiki).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam Mkurugenzi wa Usimamizi wa Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Brigedia Jenerali Hosea Ndagala alisema kushughulikia tatizo la Uvida pamoja na Zuonotiki kunahitaji ushirikiano wa pamoja.

Alisema: "Kampeni ya "Holela-Holela Itakukosti," ambayo inamaana ya 'uzembe unagharimu' inaonyesha uhusiano muhimu kati ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira. Kwa kutumia mkakati wa sekta mtambuka, inalenga kushughulikia sababu mbalimbali za kijamii".

Brigedia Jenerali Ndagala alisema tabia duni za ufugaji, kama vile msongamano wa wanyama na udhibiti duni wa magonjwa, husababisha milipuko ya mara kwa mara ya magonjwa ya kuambukizwa kwa wanyama.

Alisema hali hiyo inasababisha wafugaji kutumia dawa mara kwa mara na hivyo kuchangia kuongezeka kwa tatizo la Uvida. Kadhalika, alisisitiza kwamba uharibifu wa mazingira na usimamizi mbaya wa taka huchochea zaidi kuenea kwa vijidudu vinayosababisha magonjwa sugu na vimelea vya vinayosababisha magonjwa ya wanyama, hivyo kuleta maambukizi yanayoathiri wanyama na binadamu.

Alisema kampeni hiyo itasambaza vifaa vitakavyotumiwa na wanahabari, waelimishaji katika ngazi ya jamii, watoa huduma za afya na viongozi wa dini.

Alisema nyenzo hizo zina taarifa ya kutosha kuhusu uhusiano kati ya afya ya binadamu, wanyama na mazingira na kuhamasisha tabia za kujikinga na Uvida na Zuonotiki.

Kaimu Mkurugenzi wa USAID, Alex Klaits, alisema: "Kampeni inaonyesha jukumu muhimu la ushirikiano katika kuleta athari chanya na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu, ikiwaleta pamoja wadau wa afya moja kutoka sekta mbalimbali kupambana na tatizo la usugu wa dawa dhidi ya vimelea".

Mkurugenzi Msaidizi wa Afya Moja, Dk. Salim Manyatta kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema: "Wafugaji wanapaswa kuboresha mbinu za ufugaji wanyama na kuhakikisha wanafuata ushauri wa wataalamu wa mifugo. Hiyo ni mbinu muhimu zaidi dhidi ya Uvida na Zuonotiki.

# Wajumbe Baraza la Wawakilishi watakiwa kuwa mabalozi wa kodi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Raya Issa Mselem, amewataka wajumbe wa baraza hilo kuwa mabalozi wa kupeleka elimu kwa wananchi kuhusu ulipaji wa kodi.

Alitoa wito huo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Utalii na Kilimo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema kodi haitakiwi kulipwa kwa nguvu, hivyo elimu ikitolewa kwa wananchi itarahisisha ukusanyaji kodi, kuwataka wajumbe hao kujua haki na wajibu wa mlipa kodi na misingi ya utozaji wa kodi.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu, kwamba wajumbe watapata ufahamu wa masuala ya ukusanyaji wa kodi pamoja na mpango mkakati wa miaka mitano.

"Tuwashukuru wenzetu wa TRA na ZRA kwa kuona umuhimu wa kuwapa mafunzo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambapo yataongezea ufahamu wa ukusanyaji wa kodi," alisema Katibu huyo.

Naye Naibu Kamishna wa TRA, Saleh Haji Pandu, alisema kuwa duniani ili serikali iendelee inahitaji fedha kupitia kodi na serikali inakusanya kodi katika maeneo makuu matatu.

Aliyataja maeneo ni wafanyabiashara wanapopata faida kutokana na ajira, uwekezaji na wafanyabiashara wanatakiwa kulipa kodi kutokana na faida zao.

Alisema eneo la pili ni uingizaji au utoaji wa bidhaa nje ya nchi ambapo jukumu hilo imepewa TRA katika kukusanya kodi hizo katika maeneo hayo na eneo la tatu mtu yoyote ambaye ananunua huduma anatakiwa kuchangia kodi.

Meneja Elimu na Mawasiliano wa TRA, Paul John, alisema mapato ya nchi ni uti wa mgongo wa uendeshaji wa shughuli za serikali na taifa haliwezi kusonga mbele kama wananchi watakuwa hawalipi kodi.

Baadhi ya wajumbe wa baraza hilo, walisema kuwa kuna changamoto kubwa ya udanganyifu kwa wafanyabiashara katika manunuzi hasa pale wananchi wanapodai risiti ambapo katika risiti hizo haoneshi matumizi halisi.




Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One, David Mayunga (kulia), akisaidiana na Msemaji wa Kampuni hiyo, Wakili John Magoti (kushoto) kumtwisha ndoo ya maji Tausi Juma, mkazi wa Urambo baada ya kampuni hiyo, kukabidhi kisima cha maji kwenye kitongoji cha Kitega Uchumi wilayani humo. . **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni ya ujenzi 'yamchefua' Makamu wa Rais

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema haridhishwi na utendaji kazi wa Kampuni ya Fuchs Construction inayojenga Shule ya Sekondari Makunduchi.

Amesema kampuni hiyo inasababisha kuchelewa kumalizika kwa wakati kwa mradi huo na kuwataka makandarasi kuutumia muda wa makubaliano uliopangwa kwa kumaliza ujenzi, ili wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa shule hiyo iliyopo Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema serikali imeamua kuwapa makandarasi wazawa kujenga majengo ya shule za ghorofa ili kuwasaidia katika utendaji kazi, hivyo ni lazima kuthamini juhudi za serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi sambamba na kuwatatulia changamoto zote zinazowakabili.

Hemed alisema kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo kutasaidia kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi kwa kukosekana mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia ikiwamo kufuata mbali elimu ya sekondari.

Akizungumzia suala ajira, alisema kuwa ameshauagiza uongozi wa Wizara ya Elimu kutoa kipaumbele cha ajira kwa vijana wazawa wa mkoa husika uliopitiwa na miradi ya elimu, ili kupunguza changamoto ya kuajiri walimu wanaotoka mbali.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema nia ya serikali ni kuhakikisha wanawaajiri walimu wazawa wanaoishi katika maeneo jirani na shule ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kutengeneza mazingira rafiki ya kujisomea.

Alisema ni vyema makandarasi wa ujenzi wa shule hiyo kutoka kuzitumia changamoto walizo nazo kuwa ni fursa kwao, ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kuishawishi serikali kuwapatia miradi mengine inapotokezea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMANI BAHATI MASADU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1287.0020.2019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **RUDI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIG/RB/127816/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NOTKA ANACLETH BANTEZE** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE641904** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi (UHAMIAJI) DAR ES SALAAM mwaka 02 OCT,2023
Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **PHQ/TAN/TAN/4878/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ADOLPH M MULEMBA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3093-0010** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KANANURA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1072-0513** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KAMENE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012 na cheti cha chuo chenye namba ya usajili **BHRA/T-2012/109** kilichotolewa **INSTITUTE OF SOCIAL WORK** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/95763/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JENIPHER RICHARD KIMANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma ya CLINICAL MADICINE Chenye No. **0148181.** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia CHUO CHA AFYA MVUMI mwaka 2023, Cheti hiki kimepotea Jijini Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/17816/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11949 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late AUGUSTINO PETER NGANUNG'A of KIZOTA**

**Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NAEMI AUGUSTINO NGANUNG'A**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 06 Day of 06, 2024
Dated at Dodoma this 24 Day of 5, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**HAMZA AHMED MAKAME** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye usajili namba **MC 707 CLA, MC 187 CAM, MC 187 BYX na MC 769 CEY.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/TAN/TAN/4878/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 1336 YA MWAKA 2023**
**BAINA YA**
**MAIMUNA MUSTAFA ........................ MDAI**

**VERSUS**

**MAHAMUDU OMARI SAID .................... MDAIWA**

**KWA: MAHAMUDU OMARI SAID**

**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Dodoma wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 28.05.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 05 ya mwezi DISEMBA, 2023.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11796 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late JEMA MACHEHO NYUGWI of CHIKOWA**
**Within Dodoma City.**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DONALD LEONARD MITI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **24 Day of JUNE, 2024**
Dated at Dodoma this **23 Day of May, 2024.**

RESIDENT MAGISTRATE

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**SUMMONS BEFORE THE COMMISSION FOR MEDIATION AND ARBITRATION**
**(HATI YA WITO MBELE YA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI)**
**(Made under Regulation 34(1)) ( Imetengenezwa chini ya kanuni ya 34(1))**

**Labour Dispute No. ( Mgogoro wa kikazi Na.) CMA/DSM/LLA/677/2023**

**Between/Baina ya BAKARI SEFU MASANGA......... Applicant (Mlalamikaji/Mwombaji)**

**And/Na**

**MEDTRONIC AG............... Respondent ( Mlalamikiwa/Mjibu Maombi**

**NOTICE TO ATTEND MEDIATION/ ARBITRATION HEARING**

**(TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI/UAMUZI)**

Take notice that the above mentioned Mediation/Arbitration has been fixed for hearing on .....day of....year 2024 at.... hours at **DAR ES SALAAM ZONE, AKIBA – BIBI TITI ROAD** (Unaarifiwa kuwa shauri lililotajwa hapo juu linalokuja kwa hatua ya usuluhishi/uamuzi, limepangwa kusikilizwa tarehe 07 Mwezi 06 Mwaka 2024 saa 6.00 mchana mahali K**ANDA YA DAR ES SALAAM, AKIBA-BARABARA YA BIBI TITI)**
You are required to appear before the commission in person and or accompanied by an advocate/personal representative as instructed and produce on that day all relevant documents you intend to rely upon in support of your defence. You are further cautioned to remain in attendance until permitted by the commission ( unatakiwa kufika binafsi ama kwa kuambatana na wakili/mwakilishi wako mbele ya Tume kamaulivyoagizwa. Unapaswa kuleta vielelezo/nyaraka muhimu unazo kusudia kuzitumia katika utetezi wako. Unatahadharishwa usipuuze kutii wito huu na unatakiwa kubakia kwenye majengo ya Tume mpaka utakapo ruhusiwa kuondoka na Tume).
Given under my hand and seal of the Commission, this..................day of .......................year 2024 ( imetolewwa na kugongwa muhuri wa Tume leo tarehe 10.................. Mwezi 05 Mwaka 2024)

NOTE APPEAR FOR AWARD DELIVERY

MUAMUZI / ARBITRATOR
TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)
10/5/2024

**IN THE DISTRICT COURT OF MOSHI**
**AT MOSHI**

**APPLICATION FOR EXCUTION NO. 1 OF 2024**

**HUBERT WALTER NGUMA........................APPLICANT**

**VERSUS**

**ICHIKAEL LEONARD MALISA...................RESPONDENT**

**TO: ICHIKAEL LEONARD MALISA .**

**NOTICE FOR MENTION,**

**TAKE NOTICE** : That the above case has been fixed for mention in the District Court of Tanzania at Moshi on 6th June ,2024 at 09:00 a.m. before Honourable P.G.MUSHI-SRM.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 9th day of May , 2024.

SGD. P.G. MUSHI
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 17 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late APAUKUNDI JOSEPH MREMA of Osterbay Area**

**Within Dodoma City Council.**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SALVATORY JOSEPH MREMA AND JESCAR JOSEPH MREMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of June, 2024
Dated at Dodoma this 24 Day of May, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:
PETITIONERS
KIMARA
UBUNGO DISTRICT
P.O.BOX ......
DAR ES SALAAM

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUSIHI Mkoa D,SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 743 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SAIF ALLI MBONDE WA MTONI**

**KATIKA SHAURII LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHABANI SEIF MBONDE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 mwezi 6 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo 23 Mwezi 5 Mwaka 2024.


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 – 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Serikali ya mpito sasa kuongoza hadi 2029

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

SERIKALI ya mpito ya Burkina Faso, imeongezwa muda kwa miaka mitano, baada ya kupitishwa kwa katiba iliyofanyiwa marekebisho katika mkutano wa kitaifa wa mashauriano.

Kiongozi wa mapinduzi ya kijeshi, Kapteni Ibrahim Traoré alitia saini mkataba huo uliorekebishwa mjini Ouagadougou, mwishoni mwa wiki na kuongeza muda wake wa kukaa madarakani zaidi ya kipindi cha awali cha miezi 21.

Marekebisho makubwa katika mkataba huo yamemtambulisha Kapteni Traoré, kama Rais wa Burkina Faso na kiongozi Mkuu wa Jeshi la kitaifa kwa muda wa serikali ya mpito, kuanzia Julai 2, mwaka huu.

Washiriki katika mkutano wa mpito wa kitaifa pia walikubali kwamba Traoré, Waziri Mkuu na Rais wa Bunge la Kutunga Sheria, watashiriki uchaguzi ujao mwishoni mwa kipindi cha miezi 60, serikali ya mpito itakapomaliza muda wake. Maamuzi yaliyotolewa wakati wa mashauriano ya kitaifa yalifanyika haraka na baadhi ya ripoti za vyombo vya habari za ndani, zikionyesha kutokuwapo kwa vyama vya siasa mwanzoni mwa mkutano.

Burkina Faso, imekuwa chini ya utawala wa kijeshi tangu 2022, ikikabiliwa na changamoto katika kudhibiti waasi wa Kiislamu, wanaohusishwa na al Qaeda na Islamic State.

*BBC*



Kapteni Ibrahim Traoré. **PICHA: BBC**

# Waandamana kudai Netanyahu ajiuzulu

**TEL AVIV,** ISAREL

MAELFU ya Waisraeli wameandamana katika miji mbalimbali, dhidi ya serikali ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, wakitaka makubaliano ya kuwarejesha mateka wa Israel huko Gaza.

Aidha, familia za mateka zinamtaka Waziri Mkuu huyo, ajiuzulu.

Kulingana na gazeti la Kiebrania Haaretz liliripoti, maandamano hayo yalifanyika siku chache, baada ya kutolewa kwa video inayoonesha sehemu ya kutekwa nyara kwa ambao walichukuliwa mateka siku hiyo.

Maandamano hayo yalianza Tel Aviv, Haifa, Jerusalem, Beersheba na karibu na makazi ya kibinafsi ya Netanyahu, huko Caesarea.

Polisi wa Israel, waliwakamata waandamanaji kadhaa, kulingana na picha zilizosambazwa kupitia mashirika ya habari.

Jeshi la Israel, limeendelea kushambulia kwa mabomu Ukanda wa Gaza na maeneo ya mji wa Rafah, siku chache baada ya Mahakama ya Kimataifa ya Haki, kutoa amri inayoitaka Israel kusitisha mashambulizi yake dhidi ya Rafah na kuruhusu misaada ya kibinadamu kuingia.

Madaktari wa Kipalestina, walisema kuwa zaidi ya watu 40 waliuawa katika mashambulio hayo katika maeneo tofauti ya Ukanda huo. Wakati huo huo, mwishoni mwa wiki, Msemaji wa Brigedi za Al-Qassam Abu Ubaida, - tawi la kijeshi la Hamas, ametangaza kuwakamata wanajeshi wa Israel katika Ukanda wa Gaza.

Alisema, katika hotuba yake iliyorekodiwa, kwamba wapiganaji wa Al-Qassam walifanikiwa kuwakamata wanajeshi kaskazini mwa Ukanda wa Gaza, kwa kuwarubuni wanajeshi wa Israel kwenye moja ya handaki.

Alisema kwamba hali za wanajeshi waliokuwa kwenye handaki ni kati ya waliofariki, waliotekwa na kujeruhiwa.

Abu Ubaida aliendelea: “Mujahidina wetu waliweza kukamata wanajeshi wa Israel, kutoka katika kikosi kilichoko kambi ya Jabalia.

Aliongeza kuwa vikosi vya Al-Qassam, walifanya makumi ya operesheni dhidi ya wanajeshi wa Israel katika kipindi cha zaidi ya wiki mbili, huko Rafah na Beit Hanoun - Erez. Hata hivyo, Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, alikanusha habari hizo kwenye akaunti yake ya mtandao wa X, akisema: „Ufafanuzi: Hakuna tukio la kuwateka nyara wanajeshi.“

*BBC*

## Watoto wachanga wafariki dunia kwa moto hospitalini

**DELHI,** INDIA

INAKADIRIWA watoto wachanga sita, waliotoka kuzaliwa, wamefariki dunia kutokana na moto katika hospitali moja huko Delhi, kulingana na polisi.

Moto huo ulizuka Jumamosi jioni katika hospitali moja eneo la Vivek Vihar katika mji mkuu wa India.

Kulikuwa na watoto 12 katika kitengo hicho, Ofisa Mkuu wa Polisi, Surendra Choudhary, alisema. Mwingine alifariki kabla ya moto kuanza.

Mamlaka ilisema hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa hospitali hiyo aliyetoroka.

Picha za kusikitisha kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha milipuko kadhaa ya moto ukiwa umeteketeza jengo zima.

Waziri Mkuu wa Delhi, Arvind Kejriwal alisema moto huo unahuzunisha moyo.

„Sababu za tukio hilo zinachunguzwa na yeyote atakayehusika na uzembe huu hataachwa nje,“ Kejriwal alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Zimamoto mjini Delhi, Atul Garg, ameliambia shirika la habari la Press Trust of India kwamba, lori 14 za zimamoto zilitumwa kukabiliana na moto huo.

„Moto ulisambaa kwa kasi sana kutokana na mlipuko wa mtungi wa oksijeni,“ alisema.

*BBC*

## Watu 15 wafariki kwa mafuriko

**BADAKHSHAN,** AFGHANISTAN,

MVUA kubwa inayoendelea kunyesha nchini Afghanistan, imesababisha vifo vya watu 15 wakiwamo watu 10 wa familia moja, kaskazini mashariki mwa nchi hiyo.

Familia hiyo, inayojumuisha wazazi na watoto wao wanane, wanaripotiwa kupoteza maisha eneo la Faizabad, mji mkuu wa mkoa wa Badakhshan.

Mkurugenzi wa idara ya kukabiliana na majanga katika mkoa huo, Mohammad Akram, alisema timu ya uokoaji imefanikiwa kuupata mwili wa mama pekee.

Mafuriko na mvua zimesababisha uharibifu mkubwa ikiwamo maafa ya mamia ya watu katika sehemu nyingi ya nchi hiyo ya bara Asia.

Shirika la Mpango wa Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), limetahadharisha kuwa manusura wanakabiliwa na hali mbaya ya kibinadamu.

*DW*

## Clara aitwa Twiga Stars kuzivaa Mali na Sudan

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya muda mrefu, hatimaye mshambuliaji Clara Luvanga anayecheza soka la kulipwa katika klabu ya Al Nasri FC ya Saudi Arabia, ameitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars kwa ajili ya michezo miwili ya kirafiki iliyo kwenye kalenda ya FIFA.

Clara ni mmoja wa wachezaji 22 walioteuliwa jana na Kocha Mkuu, Bakari Shime kuwavaa Sudan Kusini na Mali katika michezo ya kirafiki inayotarajiwa kupigwa mwishoni mwa mwezi huu.


Kwa muda mrefu mchezaji huyo amekuwa akikosekana katika kikosi cha timu ya taifa kiasi cha mashabiki wengi wa soka kuwa na maswali mengi ya kujiuliza bila kupata majibu.

**Shime amewataja wachezaji wanaotarajiwa kuingia kambini hivi karibuni kuwa ni, Najat Abbas, Lidya Mrisho, Christer Bahera, Jeneth Pangamawe, Joyce Lema, Jamila Rajab, Winifrida Gerald, Stumani Abdallah, na Alia Fikiri, wote hao kutoka JKT Tanzania.**

Wengine ni Vaileth Nicholaus na Aisha Juma kutoka Simba Queens, Asha Mrisho kutoka Amani Queens, Adha Ramadhani kutoka, Yanga Princess, Julietha Singano akitokea klabu ya Juarez ya Mexico, Enekia Kasonga wa Eastern Flames ya Saudi Arabia, Maimuna Kaimu anayeichezea ZED FC, ya Misri, Suzan Adam wa Tuthankhamun ya Misri, Ester Maseke akitokea Bunda Queens, Diana Lucas wa Ame S.F.K, ya Uturuki.

Wengine ni Nahodha wa kikosi hicho, Oppa Clement anayeichezea Besiktas ya Uturuki, Aisha Masaka wa BK Hacken ya Sweden na Clara ambaye anacheza soka la kulipwa nchini Saudi Arabia.

**Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC, Waziri Barnabas (kushoto), akikabidhi tuzo kwa mchezaji wa Yanga, Aziz Ki aliyetangazwa mchezaji bora wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara kwa mwezi wa Aprili. Makabidhiano hayo yalifanyika mapema kabla ya mchezo wa Ligi Kuu kati ya Yanga SC dhidi ya Tabora United uliofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## KUOGELEA TAIFA KUFANYIKA JUNI 22

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Taifa ya watoto ya mchezo wa kuogelea (Tanzania National Junior Championship) yamepangwa kufanyika Juni 22 na 23 mwaka huu kwenye bwawa la kuogelea katika Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST), Masaki jijini Dar es Salaam imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa ufundi wa Chama cha Mchezo huo hapa nchini (TSA), Amina Mfaume, alisema lengo la mashindano hayo ni kuinua vipaji vya vijana ili wapate uzoefu wa kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Mkurugenzi huyo alisema mashindano hayo yatashirikisha klabu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na Visiwani Zanzibar.

"Maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vizuri, watoto wote wanaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kuiweka sawa miili yao, alisema Mfaume.

Alisema kupitia mashindano hayo wanatarajia kupata vijana wenye uwezo na kuomba Watanzania pamoja na wadau wa mchezo huo wajitokeze kwa wingi kushuhudia vipaji vitakavyoonyeshwa siku hiyo.

Wakati huo huo, Rais wa Chama hicho, Mhandisi David Mwasyoge, alisema mashindano hayo yatashirikisha watoto zaidi ya mia moja na kuomba wadau mbali mbali wajitokeze kuwaunga mkono, kwani kuendesha mashindano makubwa kama hayo hutumia gharama kubwa.

"Tunaomba taasisi na wadau mbalimbali wajitokeze kutuunga mkono ili tuweze kufanikisha mashindano haya ambayo yatagharimu kiasi kikubwa cha fedha, alisema Mwasyoge.

Alisema mwanzoni mwa mwezi ujao ndio watajua idadi kamili ya klabu zilizothibitisha kushiriki na kuwafahamisha wadau na wapenzi wa mchezo huo wafahamu kinachoendelea.

Aidha, aliomba Watanzania wampigie kura Mkurugenzi wa ufundi, Amina Mfaume kwenye tuzo za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambaye anawania nafasi ya kocha bora na Katibu Mkuu wa zamani wa chama hicho, Noel Kiunsi anayewania tuzo ya mwamuzi bora.

==

# MKUDE
## AFURAHIA UBINGWA KUMFUATA KILA TIMU

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji wa Yanga, Jonas Mkude, ameeleza kufurahishwa kwake kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kila timu anayohamia, akisema ni bahati kwake katika historia yake ya soka nchini kwani si kila mchezaji anaipata.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa kombe la ubingwa kwa timu yake, kiungo huyo wa zamani wa Simba, alisema anajihisi mwenye bahati kubwa, kwani kuna wachezaji wakubwa nchini lakini wamestaafu hawajapata ubingwa, au wamepata wakiwa na timu moja tu.

Juzi, Yanga ilikabidhiwa kombe lao la ubingwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya mchezo dhidi ya Tabora United ambao waliibuka na ushindi wa mabao 3-0.

"Ni faraja kwangu kwa sababu si rahisi kwa mchezaji kupata historia kama hiyo na uzuri wa historia inaishi, vizazi vinavyokuja baadaye vitakuja kusoma kuwa kuna mtu alipita alifanya mambo haya," alisema Mkude.

Ubingwa huo unakuwa wa sita kwa Mkude kuupata, mara tano akiwa na klabu ya Simba, msimu wa 2011/12, baadaye msimu wa 2017/18, 2018/19, 2019/20 na 2020/21, kabla ya kuupata msimu mmoja tu baada kuhamia Yanga.



Alisema ubingwa wa msimu huu ni maalum kwa familia yake hasa mama yake ambaye ndiye kila kitu kwake, lakini akasikitika kutokuwapo kwa baba yake mzazi ambaye angefurahia zaidi ubingwa huo kwani alikuwa ni shabiki wa Yanga.

"Ubingwa huu nautoa kwa familia yangu tu, mama yangu mzazi, nasikitika tu baba yangu mzazi angekuwa hai angefurahi sana kwa sababu hii ni timu yake aliyokuwa anaipenda, kwa bahati mbaya ametangulia mbele za haki," alisema Mkude.

Mchezaji huyo ni zao la kikosi cha vijana cha Simba, na mara ya kwanza alipandishwa na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2011/12 ambao Simba ilitwaa ubingwa.

## ZISIKUPITE

### DE BRUYNE KUBAKI CITY

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne anatarajiwa kuongeza mkataba wake Manchester City licha ya washauri wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kufanya mikutano na klabu za Saudi Arabia. ***(Mirror)***

### DIAZ ANYATIWA BARCA

MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Deco anavutiwa na winga wa Liverpool, Luis Diaz na klabu hiyo ya Hispania inaweza kumuuza fowadi wa Brazil Raphinha ili kupata fedha za kumnunua nyota huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye miaka 27. ***(AS)***

### TEN HAG HAKIELEWEKI

MMILIKI mwenza wa Manchester United Sir Jim Ratcliffe hakujibu swali alipoulizwa iwapo kocha Erik ten Hag atasalia katika kazi yake kufuatia ushindi wa timu yake katika fainali ya Kombe la FA dhidi ya Manchester City. ***(Mail)***

### BOWEN ANATAKA KUBAKI

MSHAMBULIAJI wa England, Jarrod Bowen anataka kusalia West Ham huku Newcastle United ikihusishwa kutaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

### ROWE KUAMUA HATIMA

KAMBI ya kiungo wa kati wa England, Emile Smith Rowe, itafanya mazungumzo na Arsenal kuhusu mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 katika klabu hiyo kufuatia muda wake mdogo wa kucheza msimu wa 2023-24. ***(CaughtOffside)***

### ALCANTARA AWINDWA BARCA

BARCELONA imewasiliana na kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara, ambaye ataondoka Liverpool mkataba wake utakapomalizika Juni 30. ***(AS)***

### KVARATSKHELIA APEWA OFA

KLABU ya PSG imetoa ofa ya euro milioni 100 kwa mshambuliaji wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 akiwa bado hajaafikiana na klabu yake ya Napoli juu ya kuongeza mkataba mpya. ***(Gazzetta dello Sport)***

### YORO AGOMBEWA

PSG wanahofia kuwa nyuma ya Liverpool, Manchester United na Real Madrid katika mbio za kumsajili beki wa kati wa Lille, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2024-25**.** ***(L'Equipe)***

### NEWCASTLE YATAKA WAWILI

KLABU ya Newcastle United inatazamia kukamilisha usajili wa walinzi wawili wa England, Lloyd Kelly wa Bournemouth mwenye miaka 25 na Tosin Adarabioyo wa Fulham mwenye miaka 26. ***(Football Insider)***


### DIPEPA AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Port Vale, Baylee Dipepa mwenye umri wa miaka 17. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England pia anasakwa na Newcastle United, West Ham, RB Leipzig, Borussia Dortmund na Aston Villa. ***(Mail)***

### CONTE ATAKIWA NAPOLI

KLABU ya Napoli inawasiliana na Antonio Conte kuhusu kocha huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur na Chelsea kuchukua nafasi ya kuwa kocha wao mpya. ***(Sky Sports Italia)***

## DON… SOKA MA… ULAYA




# PSG YAMWINDA BERNARDO SILVA

●●● Imepanga kumsajili nyota huyo katika kipindi hiki cha majira ya joto ili…

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-German (PSG) bado ina nia kubwa ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva na wanaweza kujaribu kumvuta kutoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 aliisaidia City kubeba taji lao la Ligi Kuu kwa mwaka wa nne mfululizo, ikiwa ni mara ya sita kwa Silva kubeba taji hilo katika misimu saba ndani ya klabu hiyo.

Kiungo huyo mkabaji anatambulika kama mmoja wa wachezaji bora anayetamba katika kikosi ambacho kina wachezaji kama Kevin De Bruyne na Phil Foden, lakini amekuwa akihusishwa kutaka kuondoka Etihad.

Barcelona pia inamtaka Silva kwa muda mrefu lakini hawajawahi kuwa katika hali nzuri ya kifedha kuweza kutoa ofa huku PSG pia wakithamini kipaji cha Mreno huyo kwa muda mrefu.

Katika madirisha yaliyopita, Manchester City walikuwa wamemthaminisha Silva kwa pauni milioni 80 na hawakuwa na nia ya kumuuza.

Silva alitia saini mkataba wa nyongeza hadi Juni 2026 mwezi Agosti mwaka jana, ambao unajumuisha kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 50 ambacho kitaanza kutumika mwaka ujao, lakini bado analengwa na PSG ambayo inajiandaa na maisha bila Kylian Mbappe.

Iwapo Silva anaweza kushawishiwa kuondoka City au la, bado haijajulikana na huwenda timu hiyo ikachukua ofa ya angalau pauni milioni 63.8.

# TEN HAG ATUMA UJUMBE BODI YA MAN UNITED

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag amelenga kutuma ujumbe kwa wamiliki wa Manchester United ikiwa hawataki awe kocha wao, atashinda mataji kwenye klabu nyingine.

Ten Hag alinyanyua kombe lake la pili baada ya misimu mingi ndani ya Old Trafford kutokana na ushindi wa kushangaza wa mabao 2-1 wa United dhidi ya Manchester City kwenye fainali ya Kombe la FA Jumamosi.

Mholanzi huyo alisema bado yuko gizani kuhusu iwapo atasalia kuwa kocha msimu ujao, lakini akasisitiza kuwa ataendelea kushinda mataji iwe yuko United au kwingineko.

„Mataji mawili ndani ya miaka miwili sio mbaya, fainali tatu ndani ya miaka miwili sio mbaya," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa baada ya mechi Jumamosi.

„Ikiwa hawanitaki, basi ninaenda mahali pengine kushinda makombe kwa sababu ndivyo ninavyofanya."

Mustakabali wa Ten Hag uko shakani kufuatia kumaliza kwa kusikitisha katika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu England.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba wakuu wa klabu wanawawania kupata saini ya Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Kieran McKenna au Thomas Frank ikiwa wataamua kufanya uamuzi wa mabadiliko ya benchi la ufundi.



Ten Hag, hata hivyo, alisisitiza kuwa anaungwa mkono na Ratcliffe na timu yake ya Ineos, inayoongozwa na mkurugenzi wa michezo Sir Dave Brailsford.

„Hicho ndicho wanachoniambia kila wakati," alisema. „Ni lazima nikuambie mara ngapi? Kila wakati ni swali moja. Je, ni lazima nijirudie mara 10, 15, 20?

„Si lazima waniambie kila wiki ikiwa wananiambia mara kwa mara. Nilisikia mara nyingi."

Ten Hag pia aliulizwa kama alihisi kuhujumiwa na United kufanya mazungumzo yasiyo rasmi na wawakilishi wa watu wanaoweza kuchukua nafasi yake kabla ya kutoa utetezi mkali wa utawala wake.

„Sijui kama wamefanya hivi, siwezi kujibu swali hili," alisema. "Sijui labda una vyanzo, mimi sina.

„Mimi nipo kwenye mradi na tupo pale tunapotaka kuwa, tunatengeneza timu kwa ajili ya siku za usoni. Nilipochukua nafasi tulikuwa tunakua, timu inashinda na timu inacheza kwa kishindo.

„Kuna kazi kubwa ya kufanya lakini tuna thamani kwenye kikosi, uwezo wa juu. Timu inaendelea na tunashinda makombe."

Nahodha wa United, Bruno Fernandes alisema wachezaji wanafahamu uvumi kuhusu mustakabali wa Ten Hag lakini akasema sio nafasi ya wachezaji kupima kile ambacho bodi inapaswa kufanya.

Katika mahojiano na ESPN baada ya mechi, Fernandes alisema: „Huu uvumi huwa unatufikia.

„Hakuna aliyekuwa na wasiwasi kuhusu hilo. Leo (juzi) tulikuwa na nafasi nzuri ya kushinda Kombe la FA, jambo ambalo ni muhimu sana nchini England. Lengo lilikuwa kwenye fainali, hakuna aliyekuwa na wasiwasi kuhusu hilo."

## Enrique: PSG itashinda Uefa licha ya Mbappé kuondoka

**PARIS,** UFARANSA

LUIS Enrique amesema kikosi chake cha PSG na usajili wao wa majira ya joto watalazimika kuongeza kasi baada ya kuondoka kwa Kylian Mbappé, lakini akasisitiza kuwa ni suala la muda kabla ya klabu hiyo kushinda taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Enrique alikuwa akizungumza baada ya ushindi wa fainali ya Coupe de France Jumamosi dhidi ya Lyon, wakati Mbappé alipocheza mchezo wake wa mwisho kabla ya kuhamia Real Madrid.

Mhispania huyo alimfundisha Mbappé katika kipindi cha mwisho cha miaka saba akiwa na PSG, kipindi ambacho mshambuliaji huyo alifunga mabao 256 na kuisaidia timu hiyo kushinda mataji 15, yakiwemo mataji sita ya ligi.

Enrique, ambaye aliiongoza PSG kutwaa mataji matatu ya nyumbani katika kampeni yake ya kwanza kuinoa, alisema sasa ni muda muhimu katika kuandaa kikosi chake kutimiza matarajio katika muhula ujao kwani hakuna mchezaji anayeweza kuchukua nafasi ya nahodha wa Ufaransa.

„Nimekuwa na bahati ya kumfundisha Kylian msimu huu, imekuwa ngumu kwake baada ya miaka saba katika klabu yake na yote ambayo amefanikisha, ni vigumu kusema kwa heri," alisema Enrique akiwaambia waandishi wa habari.

„Hakuna mbadala wa Mbappé, hatuwezi kuchukua nafasi yake, tutafanya hivyo kupitia timu na wachezaji wanne, watano au sita ambao tunaweza kufanya.

„Mbadala wa Kylian atakuwa timu pamoja na mashabiki na matarajio yetu, tutajaribu kushinda kila kitu katika misimu inayofuata."

Changamoto kubwa ya PSG bado ni Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuongeza muda wa kusubiri taji lao la kwanza la Ulaya licha ya uwekezaji mkubwa kwenye kikosi kufuatia kupoteza kwao nusu fainali dhidi ya Borussia Dortmund mapema mwezi huu.

„Changamoto kubwa kwa mchezaji yeyote anayetaka kuja ni kwamba tunataka kuweka historia na klabu hii itashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema au baadaye, ni ngumu, lakini timu hii itafanya hivyo," Enrique alisema.

"Msimu huu unamalizika, lakini tayari mazungumzo yameanza na kuna uwezekano wa kuboresha kikosi, bado ni mradi wa kuvutia.

„Klabu kubwa inahitaji sana wachezaji wanaotakiwa kuzoea. Hakuna kitu kama likizo katika soka la kiwango cha juu."

## Kroos aagwa rasmi Real Madrid

**MADRID,** HISPANIA

MASHABIKI na wachezaji wa Real Madrid walimuaga rasmi Toni Kroos aliyetokwa na machozi siku ya Jumamosi wakati kiungo huyo akicheza mchezo wake wa mwisho Santiago Bernabeu kabla ya kustaafu soka msimu huu wa majira ya joto.

Kroos, ambaye alitangaza uamuzi wake wa kustaafu wiki hii alicheza dakika 87 katika mchezo ambao walitoka suluhu na Real Betis.

Huo ulikuwa mchezo wake wa mwisho kwenye ligi kwa klabu hiyo, kabla ya fainali yao ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund Juni 1.

„Siyo rahisi," alisema Kroos mwenye umri wa miaka 34, akiiambia Real Madrid TV.

"Naweza kusema asante kwa mashabiki wa Madrid, klabu, wachezaji wenzangu na uwanja huu. Siku zote nimekuwa nyumbani katika miaka hii 10 hapa. Sikuweza kuuliza zaidi. Imekuwa miaka 10 isiyosahaulika. „

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ambaye ataichezea nchi yake kwenye michuano ya Euro msimu huu wa kiangazi kabla ya kustaafu, alipokea heshima kutoka kwa timu zote mbili kabla ya mchezo huo, huku mashabiki wakibeba lililosema „asante gwiji."

Kroos alichukua kitambaa cha unahodha jioni hiyo, na wachezaji wenzake wa Madrid walivaa jezi za ‚Kroos namba 8' kabla ya mchezo kuanza.

"Ni wazi ni hisia tofauti unapojua ni mchezo wako wa mwisho," alisema.

"Nilisema nataka kufurahia na nilifanya, nilifurahia dakika hizi 85 sana, kama nimekuwa nikifurahia kucheza hapa. Unacheza kila baada ya wiki mbili hapa, lakini ni maalum sana."

Kroos alitolewa dakika ya 87 huku akishangiliwa na mkashabiki na akajumuika na watoto wake uwanjani baadaye na kupokea makofi zaidi kutoka kwa umati wa mashabiki uwanjani hapo.

"Nilikuwa na nguvu sana hadi nilipowaona watoto wangu."

Alisema, akielezea machozi yake. "Hii ni timu maalum, ni kundi zuri. Wote wamenipa heshima ambayo nadhani nilistahili. Sio wachezaji wazuri tu, ni watu wazuri."

Kroos ambaye ameshinda mataji 22 akiwa na Madrid, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya manne na mataji manne ya LaLiga atapata nafasi ya kuongeza taji lingine kwenye mkusanyiko wake Wembley wikendi ijayo.

"Nilitaka kustaafu kwangu rasmi kabla ya mchezo huu, ili kufikia kesho tuweze kusahau kuhusu mada hii," alisema Kroos na kuongeza,

"Njia bora ya kuondoka itakuwa kushinda kombe."

Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti alisema ilikuwa ni heshima inayofaa.

# LIGI KUU BARA SASA KUBORESHWA ZAIDI

**Na Faustine Feliciane**

MDHAMINI mkuu wa Ligi ya Kuu Tanzania Bara, Benki ya NBC amejipanga kufanya maboresho zaidi kwenye ligi hiyo katika miaka minne iliyosalia.

Akizungumza juzi wakati wakikabidhi kombe la ubingwa kwa klabu ya Yanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Elirehema Doriye alisema wamejipanga kuboresha ligi hiyo katika kipindi cha mkataba kama mdhamini mkuu.

"Kila mtu ni shuhuda wa mapinduzi makubwa ambayo tayari NBC tumeyafanya katika misimu hii mitatu ya udhamini wetu kwenye Ligi Kuu ya NBC na mwaka mmoja wa udhamini wetu kwenye ligi ya Championship na Ligi ya Vijana."

"Mbali na kuchochea ushindani kwenye ligi hizi kupitia udhamini ulioviwezesha vilabu shiriki kufanya usajili mzuri, pia tumekuwa tukitoa huduma muhimu kwa timu hizi ikiwamo bima ya afya, mikopo ya usafiri kwa timu na zaidi tunahakikisha tunaandaa mazingira mazuri zaidi ya kuwakabidhi vikombe vyao vya ubingwa kwa kushirikiana na vilabu husika kuandaa matukio makubwa yenye kuongeza mvuto kwa mashabiki wao," alisema.

Alisema wataendelea kuboresha ligi hiyo ili kuwa na msisimko na ushindani zaidi kwa miaka ijayo.

Aidha, Mkurugenzi wa Fedha wa Benki hiyo, Waziri Barnabas na Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Fedha, Peter Nalitolela waliongoza zoezi la kukabidhi tuzo kwa mchezaji wa Yanga Aziz Ki aliyetangazwa mchezaji bora wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara kwa mwezi wa Aprili sambamba na kocha wa timu hiyo, Miguel Gamond kuwa kocha bora wa mwezi huo.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya kombe hilo, Mkuu wa Idara ya Masoko wa Benki hiyo, David Raymond pamoja na kuipongeza timu ya Yanga SC kwa kuibuka kinara wa ligi iliyokuwa na ushindani mkubwa miongoni mwa timu shiriki, alisema benki hiyo ikiwa kama mdhamini mkuu wa ligi hiyo inaendelea kubuni mikakati mikubwa zaidi ya kuiboresha ligi hiyo ili kufikia malengo ya udhamini wake ambayo ni pamoja na kukuza vipaji na viwango vya soka nchini, kuchochea ajira kupitia michezo, kuongeza ushindani baina vilabu shiriki na kuongeza hamasa ya mchezo huo nchini.

"Kila mtu ni shuhuda wa mapinduzi makubwa ambayo tayari benki ya NBC tumeyafanya katika misimu hii mitatu ya udhamini wetu kwenye Ligi Kuu na mwaka mmoja wa udhamini wetu kwenye ligi ya Championship na ligi ya Vijana."

"Mbali na kuchochea ushindani kwenye ligi hizi kupitia udhamini ulioviwezesha vilabu shiriki kufanya usajili mzuri pia tumekuwa tukitoa huduma muhimu kwa timu hizi ikiwamo bima ya afya, mikopo ya usafiri kwa timu na zaidi tunahakikisha tunaandaa mazingira mazuri zaidi ya kuwakabidhi vikombe vyao vya ubingwa kwa kushikiriana na vilabu husika kuandaa matukio makubwa yenye kuongeza mvuto kwa mashabiki wao," alisema Raymond.

Kwa mujibu wa Raymond udhamini wa benki hiyo kwenye ligi hizo umeambatana na matokeo chanya hata nje ya mchezo husika ambapo kupitia mnyororo wa sekta ya mchezo benki hiyo imeweza kuzalisha ajira 7,000 kupitia udhamini huo.

"Ni matokeo chanya kama haya ya ongezeko la ajira na hamasa ya mchezo huu ndivyo vinavyotupa msukumo zaidi wa kuendelea kubuni mikakati mikubwa zaidi ili kupamba zaidi udhamini wetu. Tunaamini katika miaka hii minne iliyosalia katika udhamini wetu tutakuja na mambo mazuri na makubwa zaidi ikiwamo kubuni huduma bora za kibenki zinazolenga kuhudumia na kutatua changamoto za vilabu vinavyoshiriki ligi hizi," alisema Raymond.




Mratibu wa Bonanza la Mac D, Deogratius Rweyunga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) juzi jijini Dar es Salaam kuhusu Tamasha la Mac D litakalofanyika Juni 8 na kwa kuzikutanisha timu za Mac D FC na Ipp Media FC katika viwanja vya ADC Kunduchi Dar es Salaam. Kulia ni Meneja Masoko na Mawasiliano wa EB 25, Mossi Kombo na kushoto ni Mkurugenzi wa Montage Ltd, Nestor Mapunda. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Azam yaanza kujipanga kimataifa

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikikaribia kukata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, klabu ya Azam FC imeendelea kufanya usajili wake mapema kabisa baada ya kukamilisha uhamisho wa mchezaji Ever Meza kutoka klabu ya Leonnes FC ya Colombia.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imesema mchezaji hiyo anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji, aliyezaliwa Julai 21, 2000, amesaini mkataba wa miaka minne, utakaombakisha hadi 2028 kwenye viunga vya Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutia saini mkataba huo, mchezaji huyo aliwataka mashabiki wa timu hiyo kutegemea mazuri kutoka kwake kwani yeye ni mchezaji jasiri.

„Kwanza najisikia furaha kuwa mahali kama hapa, nawaahidi mashabiki wa Azam FC wategemee kitu kizuri kutoka kwangu, mimi ni mchezaji jasiri, mpambanaji na mshindani sana," alisema Meza, ambaye alikuwa anaichezea klabu ya Alianza FC ya Colombia kwa mkopo, huku klabu mama ikiwa ni Leonnes FC .

Habari kutoka ndani ya Azam FC zinasema, klabu hiyo imetumia kiasi cha takribani Sh. milioni 845 kwa ajili ya kuinasa saini ya kiungo huyo.

Meza, anakuwa mchezaji wa pili kusajiliwa kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kwani tayari klabu hiyo imemshusha beki wa kati Yoro Mamadou Diaby aliyekuwa akiichezea klabu ya Stade Malien de Bamako ya nchini Mali.

Chanzo kingine kutoka Azam, kinasema klabu hiyo huenda ikamsajili mshambuliaji wa Mashujaa FC, Adam Adam, ambaye tayari ameshaagana na timu hiyo.

Azam ina tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao, ingawa mpaka sasa haijajulikana kama ni Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho mpaka baada ya matokeo ya mechi yake ya mwisho kesho dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

## Mabingwa Yanga raha

INATOKA UK. 24

Walipowasili makao makuu ya klabu hiyo, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe alitambulisha benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi na viongozi wa kamati ya utendaji inayoongozwa na Rais, Hersi Said.

Pia walitambulishwa wachezaji wote ambao wamefanikisha kutetea taji lao kwa mara ya tatu mfululizo na kukata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Dickson Job, aliwashukuru wanachama na mashabiki wa Yanga kwa kuwa nao pamoja kwa msimu mzima na kuendelea kuwasapoti katika michezo iliyosalia.

"Bado hatujamaliza na tunakibarua kingine mbele yetu, tuna deni lingine na tunatakiwa kwenda kulilipa visiwani Zanzibar katika fainali ya kombe la Shirikisho la CRBD Bank na kurejea Dar es Salaam na kombe," alisema Job.

Aidha, Rais wa timu hiyo, Hersi alisema wachezaji, benchi la ufundi na uongozi wamefanya kazi kubwa ya kuchangia ubingwa wa 30 na kutwaa mara tatu mfululizo.

"Kila mmoja anatambua kuwa Juni 2, mwaka huu kuna kibarua kigumu sana mbele yetu na tunaenda kujenga kuhakikisha tunafanikiwa kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho na kuja kulitambulisha kwa mara nyingi hapa klabuni.

Niwaahidi mashabiki na wanachama tunaenda kujenga timu yetu bora kuliko msimu huu kwa kusajili nyota wengine wenye uwezo na hatutaacha mchezaji yeyote yule ambaye atakuwa kwenye mipango yetu," alisema Hersi.

## Mgunda: Tunasubiri

INATOKA UK. 24

wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisisitiza kuwa sasa wanasubiri mechi za mwisho kujua hatima yao.

"Malengo matatu yote yamekamilika, ilikuwa ni kuwaletea mechi mashabiki wa Arusha, pili kuona mechi yetu inakuwa na watazamaji wengi, tatu ilikuwa ni kupata ushindi na yote yametokea.

Unaweza kuwa siyo ushindi wa kuridhisha sana kwa sababu ya mbio zilizopo sasa, hatukutakiwa kushinda tu, bali kwa idadi kubwa ya mabao kwa sababu hali inavyoonekana, nafasi ya kwenda Ligi ya Mabingwa haitaamuliwa na kushinda tu, kila mtu ana uwezo wa kushinda mechi zake, kinachokwenda kutengeneza utofauti ni idadi ya mabao. Pamoja na yote mwamuzi ni mechi za mwisho," alisema Ahmed.

Mpaka sasa timu ambazo zina tiketi mkononi ya kucheza mashindano ya kimataifa ni Yanga ambayo itacheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, Coastal Union itakayocheza Kombe la Shirikisho kwa kuwa inashika nafasi ya nne kwa pointi 42 ambazo hazitofikiwa na timu yoyote iliyo chini yake. Azam iko nafasi ya pili ikiwa na pointi 66 na mabao 61, Simba ya tatu ikiwa na mabao 66 na mabao ya kufunga 57.

# Michezo

Jumatatu Mei 27, 2024

Nipashe


## PSG bado yamwinda Silva



UKURASA 21

●●● Mashabiki watamba kila kona, supu yanyweka kwa Mkapa huku wakiipania Azam kwenye...

# Mabingwa Yanga raha

**Na Saada Akida**

DAR ES SALAAM ni kijani na njano, kwa sasa hakuna rangi ambayo imetawala zaidi ya rangi hizo baada ya Yanga kukabidhiwa kombe lao la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara juzi.

Ubingwa huo wa Yanga msimu huu unakuwa wa 30 katika rekodi ya timu hiyo na kuzidi kuwaacha mbali watani zao Simba.

Yanga walikabidhiwa kombe lao juzi baada ya mchezo wao dhidi ya Tabora United uliochezewa Uwanja wa Benjamin Mkapa na kufanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Yanga waliendeleza sherehe zao jana kuanzia saa 4:00 asubuhi kwa mashabiki wao kunywa supu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo kulianzia shamra shamra za kusherehekea ubingwa.

Baada ya kunywa supu wachezaji na baadhi ya viongozi walipanda kwenye basi maalum ambalo lilibeba kombe lao la ubingwa huku wakifunga barabara kwa kulitembeza kombe hilo kutoka uwanjani mpaka makao makuu ya klabu hiyo, Jangwani.

Walipita Keko, Tazara, Buguruni, Karume. Mitaa ya Msimbazi na safari kuishia makao makuu ya klabu hiyo huku maelfu ya mashabiki walijitokeza kwenye paredi hiyo.

Yanga walitumia saa tatu na nusu kufanya paredi kutoka Benjamin Mkapa hadi makao makuu ya klabu hiyo na kufika saa 7: 30 mchana.

INAENDELEA UK. 23




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Kazi Maalum), Kapteni Mstaafu George Mkuchika (kushoto), akiwa na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NBC, Dk. Elirehema Doriye (wa pili kushoto) wakikabidhi kombe la Ligi Kuu ya NBC kwa Nahodha wa Timu ya Yanga, Bakari Mwamnyeto (kulia), baada ya timu hiyo kuwa bingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2023/2024. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## Mgunda: Tunasubiri hatima yetu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Juma Mgunda, amesema kwa hali ilivyo sasa, mechi watakayocheza dhidi ya JKT Tanzania na ile kati ya Geita Gold dhidi ya Azam FC, ndiyo itakayoamua hatima ya timu gani kati yao na Wanalambalamba hao watakwenda Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC walioibuka na ushindi wa bao 1-0, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Mgunda alisema katika mechi hiyo ya juzi walihitaji ushindi wa mabao mengi, lakini kwa bahati mbaya haikuwa hivyo, hivyo hawana la kufanya na hatima yao itaamuliwa katika mechi hizo.

"Lengo letu ilikuwa tupate pointi tatu na mabao mengi lakini haikuwa hivyo, kwa sababu hiyo ni mapema zaidi sasa kusema lolote, kilichobaki tunakwenda kwenye viwanja vya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi iliyobakia.

Ukweli ni kwamba hizi mechi ni ngumu, ikumbukwe kuwa KMC nao walikuwa wanaisaka nafasi ya nne walikuwa wanagombania na Coastal Union," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema japo timu yake ina baadhi ya wachezaji wazuri, lakini imekuwa na mapungufu mengi ambayo watayaweka hadharani ikifika wakati wa kufanya hivyo.

"Niwapongeze wachezaji wangu wamecheza vizuri, lakini timu ina mapungufu kadhaa ambayo ikifika wakati wake tutayazungumza," alisema kocha huyo aliyechukua kijiti kutoka kwa Abdelhak Benchikha ambaye alibwaga manyanga.

Aidha, Meneja Habari na Mawasiliano

INAENDELEA UK. 23

## Ten Hag atuma ujumbe Bodi ya Man United

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag amelenga kutuma ujumbe kwa wamiliki wa Manchester United ikiwa hawataki awe kocha wao, atashinda mataji kwenye klabu nyingine.

Ten Hag alinyanyua kombe lake la pili baada ya misimu

INAENDELEA UK. 22

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >